COVERINGCRSV.ORG

JINSI YA KURIPOTI KUHUSU UKATILI WA KIJINSIA KWENYE MAENEO YA MIGOGORO

Inapatikana kwa **Kiingereza, Kifaransa, Kihispania, Kiswahili** na **Kiarabu**.

© Dart Centre Europe | Toleo Moja

YALIYOMO

KUHUSU NA SABABU

#1. JE! NIMEJIANDAA VYA KUTOSHA KWA JAMBO HILI?

#2. JE! NI VIZURI KUMHOJI MTU HUYU, KWA WAKATI HUU NA MAHALI HAPA?

#3. JE! MHOJIWA WANGU ANAELEWA KIKAMILIFU WANACHOSAINI?

#4. WAPE WAATHIRIKA KUZUNGUMZA KWA NJIA WANAYOTAKA NA KWA WAKATI WANAOTAKA

#5. KUELEWA ATHARI ZA KUENDELEA ZA KIWEWE KWENYE KUMBUKUMBU NA HISIA ZA USALAMA

#6. FAHAMU JINSI HISIA ZAKO PIA ZINAHUSIANA NA MASUALA HAYA

#7. KUMBUKA: UNYANYASAJI WA KIJINSIA SIO MWELEKEO PEKEE WA HADITHI KWENYE TUKIO

#8. PICHA HAZIFUTIKI: KUWA MWANGALIFU KWA PICHA UNAZOTUMIA

KUHUSU

Kuna changamoto chache za uandishi wa habari, huenda ikawa hapana, ambayo ina uzito mkubwa wa uwajibakji kuliko kuhoji wahanga wa unyangasaji wa kijinsia kwenye maeneo ya migogoro. Ubakaji ukitumiwa kwenye migogoro, unaleta athari mbaya kwa watu binafsi na jamii zao.

Uandishi wa habari unaowajibika unaweza kuleta umakini na ufahamu kwa uhalifu ambao watu wengi wanakosa maneno ya kuueleza. Kwa upande mwingine, kuripoti kwa njia ya uzembe kunaweza kufanya mambo kuwa mabaya zaidi kwa kuongeza dhiki na kuwaweka wahasiriwa kwa hatari zaidi. Miongozo hii imeandikwa na wanahabari na watengenezaji wa filamu ambao hufanya kazi mara kwa mara kwenye maswala yanayohusiana na ukatili wa kingono katika migogoro. Miongozo hii inatokana na utambuzi kwamba, kama uanahabari kwa jumla unahitaji kufanya zaidi ili kufafanua na kufahamisha wengine mbinu bora. Lengo ni kuripoti vizuri maswala haya ambayo hupunguza hatari ya kusababisha madhara zaidi kwa wale wenye ujasiri wa kutosha kusimulia hadithi zao.

KWA NINI HII?

Miongozo hii imeibuka kutokana na mazungumzo kadhaa kati ya wanahabari wenye uzoefu na watengenezaji wa filamu ambao wamefanya kazi mara kwa mara kwa muda mrefu kwenye hadithi zinazohusu unyanyasaji wa kijinsia na mateso katika nchi zilizo athirika na migogoro.

Bila shaka kila mtu anyefanya kazi hii ana nia nzuri. Lakini wakati fulani sisisote tunaweza kujiuliza ikiwa kuna uwezekano kwamba tunaweza kuwa tuna wadhuru watu ambao hadithi zao tunajaribu kuripoti.

Wanahabari, ambao mara nyingi huwa wa kwanza kuhoji wahasiriwa wa ukatili wa kijinsia katika maeneo ya migogoro lakini mara nyingi hawapati mafunzo yoyote ya msaada ambao wanahitaji kufanya kazi hii kwa usalama na kwa ufanisi.

Ndio maana tukatayarisha muongozo huu. Miongozo hii inaangazia masuala nane muhimu ya ujuzi ambayo tuna imani kwamba kila mwanahabari au mtengenezaji wa filamu anayefanya kazi kwenye maswala yanayohusiana na ukatili wa kingono anahitaji kufahamu. Mapendekezo haya manane yameundwa kusomwa kwa kina na katika muundo unaoruhusu kutumiwa kama msingi wa mrekebisho -na kusambazwa kwa wafanyakazi wenza. Mapendekezo hayo yamekusudiwa kuwa ya manufaa na kujibu hali halisi juu ya ardhi.

Ijapokuwa mapendekezo haya yaliandikwa na wanahabari kwa ajili ya wanahabari, yametokana na mazungumzo pana. Wakati wa kuunda nyenzo hizi, tuliwasiliana na manusura wa mizozo unyanyasaji wa kijinsia (ambao wengine ni wanaharakati lakini wote ni wataalam), daktari wa maswala kiwewe, wafanyikazi wa jamii, wanasheria, wapiga picha, watengenezaji wa filamu, wanahabari na wahariri.

Hili ni swala ngumu. Wala miongozo hii haitaangazia kila hali anayokabiliwa na mwanahabari.

Hata hivyo, tumejaribu sana kusawazisha mambo haya mawili. La kwanza ni kwamba kama vitendo hivi vya ukatili havitaripotiwa, itakuwa vigumu kuvikomesha. La pili ni kwamba linapokuja suala la ukatili kingono, kila mhasiriwa ana masimulizi yake – sio sisi tunamiliki habari hizo.

KIPI KINAFUATA?

Tuliunda miongozo hii ili kutoa nafasi ya majadiliano na pia ili kuhamasiha watu. Lengo la miongozo hii ni kusambazwa Na kwa hivyo tafadhali sambaza kwa mtu yeyote ambaye anaweza kufaidika

Ikiwa unataka kujua zaidi kuhusu kazi ya Kituo cha Dart, tafadhali jiandikishe **hapa**. Tunakaribisha maoni yako na tunatarajia mazungumzo huko mbele.

SHUKRANI NA UTAMBUZI

Miongozo hii imetayarishwa na **Dart Centre Europe**, ambao ni mtandao na rasilimali kwa wanahabari na watengenezaji wa filamu ambao hushughulikia masuala ya kiwewe na vurugu. Kwanza tunatoa shukrani kwa kila mtu ambaye amechangia mazungumzo ya Kituo hiki kwa miaka hii yote. Timu kuu ya kuandaa na kuandika: **Gavin Rees**, **Samira Shackle**, **Stephen Jukes**, **Juliana Ruhfus**, **Leslie Thomas** na **Christina Lamb**.

Tunatoa shukrani pia kwa kila mtu ambaye alishiriki katika mashauriano yetu ya moja kwa moja.

DART CENTRE EUROPE

Mradi huu uliwezeshwa kupitia ufadhili wa Ofisi ya Jumuiya ya Madola ya Kigeni na Ofisi ya Maendeleo kitengo cha Mpango Kuzuia wa Ukatili wa Kijinsia.

Dart Centre Europe
Nambari ya usajili wa hisani nchini Uiengereza na Wales: 1172731
Tafadhali wasiliana nasi. Tunakaribisha maoni. **covering.crsv@dartcentre.org**

Tafadhali fikiria tu kuchapisha kurasa za nakala za greyscale

#1.

MASWALI MATATU YA MSINGI

JE! NIMEJIANDAA VYA KUTOSHA KWA JAMBO HILI?

MASWALI MATATU YA MSINGI

#1. JE! NIMEJIANDAA VYA KUTOSHA KWA JAMBO HILI?

Kuzungumza na vyombo vya habari juu ya ukatili wa kijinsia kwenye maeneo ya migogoro ni hatari kubwa kwa aliyenusurika. Miongozo hii itakupa fikra nzuri kuhusu kile kilicho hatarini.

Kuripoti kuhusu unyanyasaji wa kijinsia ni mojawapo ya kazi yenye changamoto kubwa kwa wanahabari na inahitaji uangalifu wa hali ya juu. Kabla ya kuanza, hakikisha unafanya utafiti kuhusu mambo yafuatayo:

- **Ukatili wa unyanyasaji wa kijinsia ni nini na vipi ubakaji unaathiri watu binafsi na jamii zao.**
- **Jinsi ya kuhoji wahasiriwa wa kiwewe kwa njia ya kuzingatia hisia zao.**
- **Nguvu za kisiasa na picha ya ujumla ya usalama katika eneo , mienendo ya kijinsia, pamoja na mitazamo ya kitamaduni kuhusu ukatili wa unyanyasaji wa kijinsia.**
- **Changuo lakuona ambalo unaweza kuhitaji kufanya. Je, utapiga picha au kuchukua filamu za watu. Jinsi na wapi? Je, watatambulishwa au la?**
- **Unamiliki Kiwango chako mwenyewe cha utayari wa kisaikolojia na kwanini hiyo ni muhimu.**

Tumeita mwongozo huu *Kuripoti juu ya Ukatili wa Kijinsia kwenye migogoro* lakini katika maandishi haya tunatumia kifupi kwa lugha ya kiingereza CRSV (Ukatili wa Kijinsia kwenye migogoro).

Ukatili wa Kijinsia kwenye migogoro inamaanisha vitendo vya ukatili wa kingono kama vile ubakaji, ukahaba wa kulazimishwa, ndoa ya kulazimishwa, uhasishwaji wa lazima na uhalifu mwingine kama huo ambao unaweza kuhusishwa na vita. Kwa kawaida, uhalifu huu hufanywa kwa malengo ya kijeshi au ya kisiasa yaliyotafakariwa – na kwa hivyo huingia chini ya vikundi vya kisheria vya mauaji ya halaiki na uhalifu wa kivita; lakini matukio yanaweza pia kuwa nyemelezi zaidi. Ukatili wa kingono kwenye migogoro una maana pana kuliko neno “ubakaji katika vita”. Neno hili pia linatumika kwa hali zisizo thabiti ambazo waasi, wanamgambo au vikosi vya serikali hutumia ukatili wa kijinsia kama chombo cha kugandamiza wenyeji wa eneo na kuwachochea wapiganaji. Hili hutokea kwa wanaume, wanawake na watoto.

Uhalifu huu una athari mbaya kwa walionusurika na jamii zao hasa kwa sababu ukatili huu unaweza kutenganisha uhusiano wa kijamii na kufanya watu kutengwa na familia, marafiki na majirani ambao wangeweza kutoa msaada na kusaidia kupona. Pia ina athari za kizazi kwa watoto waliozaliwa kutokana na ubakaji na inaweza kusababisha unyanyapaa unaoendelea na vurugu zaidi kwa njia ya kile kinatambulika kama mauaji ya heshima ya kibinafsi.

Jukumu letu kama wanahabari na watengenezaji wa filamu sio ujasiri

Mara nyingi wanahabari huwa wa kwanza kuhoji manusura na katika kuangazia mambo ambayo watu wanapaswa kujulishwa, wanahabari wanajipata katika hatari kubwa kibinafsi. Ingawa hakuna mwandishi wa habari anayefanya kazi hizi anayetaka kusababisha madhara kwa wale wanaowahoji bila makusudi, lakini kuna uwezekano wa madhara kutokea. Hata kwa nia njema, makosa katika kuhoji na kuripoti yanaweza kuwafanya manusura kuona

kama wametengwa na kutumiwa vibaya na pia inapelekea wahojiwa na familia zao kupatwa na aibu na hata wakati mwingine kupelekea kutendewa vurugu.

Mnamo 2018, ripoti ilichapishwa ambayo ilifanya kitu kisicho cha kwawaida kwa kuuliza wahasiriwa wa ukatili wa kijinsia katika eneo la vita tajriba yao baada ya kuhojiwa na wanahabari. Majibu yao yalikuwa ya kusisimua. Asilimia themanini na tano walikumbana na mbinu za kuripoti ambayo zilikiuka miongozo miwili bora ya wanahabari amabyo iliyochapishwa na Kituo cha Dart na yingine iliyofanywa na shirika la Umoja wa Mataifa linalofanya kazi kwa ulinzi wa wahasiriwa.[a] Masuala yaliyoainishwa katika ripoti hiyo ni pamoja na:

> *Ukiukaji dhahiri kwa njia ya ahadi za pesa au msaada, kufichua utambulisho bila idhini, au kushinikizwa kutoa maelezo ya kitendo cha ubakaji na unyanyasaji wa kijinsia, kuuliza wanawake maswali ya kibinafsi na ya kindani kuhusu mashambulio hayo. Hali kadhalika, wanahabari walionyesha ishara walikuwa katika nafasi ya kusaidia jamii ya Yazidi kwa kuchapisha habari za wanawake wahasiriwa.[b]*

Ni kawaida kwa wanahabari kupata mafunzo kuhusu mazingira ya uhasama ili kuwandaa kujiweka salama katika hali za hatari. Kwa upande mwingine, wanahabari wengi bado hawapati mafunzo stahiki na mwongozo katika kufanya kazi na wahasiriwa wa kiwewe.

Je, ni yapi maandalizi mema?

Katika safari yoyote ya kuripoti, haswa katika eneo lenye hatari kubwa, wakati ni wa thamani sana na inafaa kufikiria juu ya mambo haya mapema wakati una nafasi ya kufanya hivyo. Maandalizi ni ya aina mbili na yote ni muhimu:

1. Aina ya maandalizi yanayohitajika kabla ya kuanza safari. Kufanya utafiti wa ndani, tathmini ya hatari, na kadhalika.

2. Kujitolea kwa muda mrefu kuimarisha ujuzi wa ufundi. Hii hutoka kwa mafunzo, kujitolea kuelewa maswala na uwazi wa kutoa-na-kuchukua kushiriki maarifa na wenzako.

Maandalizi yanayohusiana na kazi maalumu

Huenda una uzoefu wa kufanya tathmini ya hatari kwa usalama wako na wa timu yako kabla ya kusafiri. (Ikiwa sivyo, tafadhali angalia kisanduku hapa chini). Wakati huo huo, wakati unaripoti kuhusu ukatili wa kijinsia, unahitaji pia kuzingatia jinsi namna ya kuripoti inaweza kuathiri usalama wa kimwili na kisaikolojia wa wale unaowahoji.

Maswali ya kujiuliza:

- Je, umechunguza mienendo ya nguvu za kisiasa na hali ya usalama kwenye eneo itakayokufanya uweze kufanya maamuzi mazuri sio tu juu ya usalama wako mwenyewe, bali pia usalama wa wale unaowahoji? [Tazama **#2**]
- Nani atawezesha mahojiano yako na manasura? Je, itakuwa mpatanishi, asasi isiyokuwa ya serikali au washawishi wa kisiasa?
- Je, unaelewa kwa undani muktadha wa kitamaduni na kidini, kilingana na ukatili wa kijinsia, na siasa za familia ili kuelewa hatari ambazo wale unaowahoji wanaeza kukumbwa nazo? [Tazama **#2]**
- Je, unafahamu sheria za mitaa katika eneo hilo na athari yoyote ambazo zinaweza kutokea kwa kufichua utambulisho wa wale unaowahoji na uwezo wao wa kutafuta hatua za kisheria ikiwa wataamua hivyo? (Katika baadhi ya mamlaka, mtu aliyebakwa anaweza kushtakiwa kwa hatia ya uzinzi).
- Je, wewe mwenyewe uko tayari kisaikolojia? Je, uko kwenye nafasi nzuri kufanya hii kazi wakati huu? [Tazama **#6**]

[a] Hizi ni miongozo ya **Kituo cha Dart** iliyochapishwa kwanza mnamo 2011. ; na miongozo kadhaa iliyochapishwa na umoja wa mashirika yasiyo ya kiseralikali, Global Protection Cluster, juu ya **kuripoti juu ya unyanyasaji wa kijinsia katika mazingira ya mahitaji ya kibinadamu**.

[b] Johanna E. Foster na Sherizaan Minwalla, 'Sauti za Wanawake wa Yazidi: Maoni ya Mazoea ya Uandishi wa Habari katika Kuripoti juu ya dhuruma, Ukatili wa Kijinsia wa Isis,' Mkutano wa Kimataifa wa Mafunzo ya Wanawake 67 (2018): 53-64.

Utayari wa kawaida

Aina nyingine ya maandalizi yanahitaji uangalifu kwa hivyo kuna mambo yanahitajika kupanga kabla ya kazi maalum. Kwa kawaida, inafaa kushiriki katika mafunzo husika lakini kama haiwezekani, kuna njia zingine kama vile kujisomea mwenyewe au ushauri mzuri kutoka kwa wenzako wenye ujuzi zinaweza kuwa muhimu sana.

Jiulize:

- Je, unayo mpango madhubuti wa usalama wa kidijitali wa kulinda wale unaowahoji wasitambulike? [Tazama kisanduku cha rasilimali **#2**]
- Je, umefanya utafiti wa mikakati wa kuhoji watu walipataa na kiwewe ambao ni wahasiriwa wa ukatili wa kingono? Kuna mambo maalum hapa ambayo unapaswa kujua. [tazama **#4** na **#5**.]
- Je, unaelewa kikamiifu idhini ifaayo, na je, umefikiria jinsi ya kuipata? [Tazama **#3**.]
- Ikiwa unapiga picha au unachukua video je, umefikiria juu ya jinsi ya kuficha utambulisho na jinsi ya kuwafanya wahasiriwa kujihisi bila wasiwasi? [Tazama **#8**.]

Mazingatio kwa wahariri

Wakati wa mchakato wa mashauriano ya kutengeneza miongozo hii, kila mtu tuliozungumza naye wakiwemo wahariri na wanahabari walio katika nchi zilizoathiriwa na ukatili na pia wale wanaoishi nje, wote walionyesha jukumu ambalo wahariri na watayarishaji wa filamu wanayo katika kulinda wanaowahoji. Wanahabari walio uwanjani hawafanyi kali bila watu wengine kwani wanawajibika kwa wakuu wa magazeti au vituo vya utangazaji.

Umbali kati ya walito ofisini na wale walio unaweza kuwa tatizo kubwa. Kwa kuwa kuna masafa kati ya chumba cha habari na pahali pa matukio, kuna uwezekano wa kukosa hisia ya kuhukumu vizuri kuhusu tukio. Lakini inaweza pia kumaanisha uelewa mdogo wa muktadha na uwezekano wa kudhuru wahasiriwa. Wakati mwingine kuna shinikizo kwa waandishi wa habari katika uwanja kupata habari kwa njia yoyote.

Vivyo hivyo, wahariri hawana habari kamili ya kile kinachotokea uwanjani. Wanahabari na watengenezaji wa filamu kawaida hufanya kazi chini ya shinikizo kubwa na wanaweza kuwa walisafiri umbali mrefu kwa hatari kubwa ya kibinafsi. Wakati mwingine wanahabari huria wanatumia pesa zao kufika katika eneo la mizozo. Katika hali hizi, wanaweza kujikuta wanatumia njia za mkato. Kwa mfano, mahojiano yanaweza kuwa ya kupindukia, kukosa kupata idhini inayofahamika kwa uzuri, kutochukua hatua za kutosha kulinda kutokujulikana kwa wahasiriwa.

Kuwepo kwa mawasiliano bora kunaweza kusaidia kuzuia hatari kama hizi. Waandishi wa habari wanahitaji kuhisi kuwa wanaweza kuwaeleza wasiwasi kwa wahariri wao, na kwamba hawataadhibiwa kwa kuweka usalama wa mwili na wa kihemko yawahasiriwa kuliko lengo la kupata habari.

Tutaangazia masuala haya kwa kina zaidi katika mwongozo huu. Lakini hapa kuna orodha fupi kwa wahariri wanaowapa wanahabari majukumu ya kuripoti habari zinazohusiana na ukatili wa kingono kwenye migogoro:

- Je, umejadili sheria za msingi waandishi wa habari wanatarajiwa kufuata wakati wa kufanya kazi na waathirika wanyonge?
- Je, umepanga vizuri namna ya kutumia picha kwa njia ambayo inaweza kulinda utambulisho na hadhi ya mwenye kuhojiwa? Hii sio rahisi kuamua kwa wakati huu.
- Je, hii kazi ni mwafaka kwa mwanahabari hivi sasa? Je, kuna hatari ya kazi nyingi kupita kiasi kutokana na kutoa ripoti nyingi kwa mfululizo?
- Je, wandishi wa habari wanafahamu kama wanaweza kujadili maswala yoyote ya kimaadili na wewe?

- Je, mwandishi ametumia muongozo kama huu?

Na mwishowe, umefikiria kutoa mafunzo yanayofaa kwa wanahabari katika kuhoji wahasiriwa wa kiwewe? Kwa bahati mbaya, hiki si kitu ambacho kawaida hujumuishwa katika mafunzo ya mazingira ya uhasama. Unaweza kupata habari zaidi kuhusu ni nini shirika lako linaweza kufanya kusaidia na kulinda wanahabari wanaoshughulikia habari zinazohusiana na kiwewe kwa kushauri **mwongozo huu**.

Sehemu ya **#7** na **#8** zinajadili masuala yanayohusika na uchapishaji na matangazo kwa undani zaidi.

Rasimali za ziada: muhtasari

Kwanza, tuanagiza kila mtu asome rasimu ya **Nambari ya Murad**. Huu ni mpango ambao unaharibu kanuni bora kabisa za mazoezi kwa mtu yeyote ambaye ana mawasiliano ya moja kwa moja na wahasiriwa wa unynyasaji wa kwenye maeneo za migogoro -iwe ni mwandishi wa habari, wakili, mchunguzi wa makossa ya jinai, mtunga sera, ao wakili ao wakili wa shirika lisilo la serkali. Ni zao la kushauriana kwa kina na vikundi vya wahasiriwa pamoja na kundi za wataalamu. Kituo cha Dart kina sehemu ya wavuti yake iliyojitolea **kufunika vurugu za kijinsia**. Huko, unaweza pia kupata kipeperushi hiki cha **Kituo kya Dart** Ulaya ambacho kinatoa muhtasari mfupi.

BONYEZA HAPA KUSHIRIKI SEHEMU HII:

Tafadhali fikiria tu kuchapisha kurasa za nakala za greyscale

#2.

MASWALI MATATU YA MSINGI

JE! NI VIZURI KUMHOJI MTU HUYU, KWA WAKATI HUU NA MAHALI HAPA?

#2.

MASWALI MATATU YA MSINGI

JE! NI VIZURI KUMHOJI MTU HUYU, KWA WAKATI HUU NA MAHALI HAPA?

Kutathmini usalama wa wanaohojiwa ni jukumu la wanahabari katika ngazi zote ikimo mwandishi aliye uwanjani, mhariri katika chumba cha habari na wenzake wanaofuatilia habari hiyo hiyo.

Wakati wa kuripoti kuhusu ukatili wa kijinsia kwenye migogoro, wanahabari wanahitaji kufanya tathmini ya hatari juu ya usalama wa wale wanahojiwa, kama vile wanavyofanya tathmini ya usalama wao wenyewe. Maswali ya msingi juu ya uangalifu unaofaa ni pamoja na:

- **Je, ninao muda wa kutosha kufanya mahojiano haya vizuri? Mazungumzo ya aina hii hayapaswi kuharakishwa. Ikiwa sivyo, nitawezaje kufanya mambo tofauti ili kuepuka kusababisha madhara yoyote?**
- **Je, mazingira haya ni salama? Nani amehudhuria kwenye chumba na ni nani hapaswi kuhudhuria? Je, ninaelewa mienendo ya nguvu za kisiasa kikamilifu ili kuweza kutathmini athari zinazoweza kutokea kwa wale ninaowahoji? Je, kuna aina yoyote ya kulazimishwa?**
- **Je, mtu huyu ndiye mtu anayefaa kuhojiwa? Je, mhasiriwa yuko tayari kihemko kufanya mazungumzo haya? Na ikiwa sio, ni nani anayeweza kuwa tayari?**

Huenda umesafiri njia ndefu kwa hatari kubwa ya kibinafsi, lakini wakati mwingine maadili ya hali yanaweza kuhitaji mpango mpya. Wahariri pamoja na waandishi walio nyanjani wanahitaji kuchukuwa jukumu la hii – Je! mazungumzo haya ya tasaidiya?

Je, ninao muda wa kutosha kufanya hii kazi?

Wanahabari hufanya kazi chini ya shinikizo kubwa la wakati. Lakini kumhoji mhasiriwa wa ukatili wa kingono unahitaji wakati wa kutosha.

- Lazima uwe na muda wa kukaa wa kutosha wa kumhoji aliyenusurika.
- Ikiwa huna wakati wa kutosha, unaweza kupanga tena siku yako?
- Je, unaweza kufanya mahojiano hayo kwa njia tofauti kwa mfano, kwa kuuliza maswali ya uhakika badala ya kumfanya mhasiriwa kuelezea fedheha aliyoipitia?
- Au unapaswa kumhoji mtu anayehusika lakini ambaye hakushambuliwa kwa nia ya moja kwa moja?

Aina hii ya mipango inaweza kuhusisha watu wengine wasiokuwa wewe mhasiriwa. Ikiwa mahojiano hayo yanapangwa kupitia mpatanishi kama vile asasi isiyo ya serikali au kikundi cha wazee wa eneo, waeleze kuhusu muda utakao kuwa nao ili uweze kupanga mambo yako ipasavyo.

Unaweza pia kumshirikisha mhasiriwa katika upangaji, kadri inavyowezekana. Ikiwa ratiba yako ni rahisi kubadilika, muulize mhasiriwa kwa mapema ikiwa kuna wakati mzuri wa kuongea, wakati ana nguvu zaidi kwa sababu yanaweza kuwa mazungumzo ya kuchosha. Kumpa mtu unayemhoji nafasi ya kubadili mpango ni njia rahisi lakini yenye nguvu ya kumfanya ajisikie kama ana udhibiti wa habari anayoitoa.

Je, mahali hapa ni salama kwa mahojiano?

Labda umezoea kufikiria juu ya usalama wa maeneo ambayo unafanyia kazi. Lakini linapokuja suala la kumhoji nusura, unapaswa kufikiria zaidi ya haya. Anza kwa kujiuliza maswali rahisi kama vile nani atakuwepo ndani ya chumba na kwa nini:

- Je, kuna watu wenye bunduki?
- Je, kuna wazee wa jamii?
- Je, kuna watu ambao wanahusiana na mitandao ya wahalifu?
- Je! Kuna mtu yeyote ambaye haitaji tu kuwa hapo?

Hata kama wahusika wa vurugu hawahudhurii kwenye chumba; jiswali piya kama wanaishi katika jamii, Je! habari kuhusu mahojiano hayo inaweza kuwafikiya?

Usirudishe wahasiriwa mahali kitendo kilitokea isipokuwa uwe unajua unachofanya. Hali hii inaweza kusababisha athari kali za kiwewe.

Ingawa inaweza kuwa vigumu kupitia hali ya aina hii, kumbuka kuwa wewe ndiye unadhibiti mahojiano, na ikiwa inaonekana imeshurutishwa, au kuna uwezekano wa kumueka mhasiriwa hatarini, unapaswa kusimamisha mahojiano hayo. Wahariri wana majukumu yao pia kwa sababu shinikizo kutoka kwa chumba cha habari linaweza kuathiri akili ya mwanabari anapokabiliwa na changamoto ya maadili.

Huenda pia kuna wasaidizi ambao umekuja nao:

- Ikiwa wewe ni mtangazaji, je, unaeza kuja na wasaidizi wachache iwezekanavyo?
- Ikiwa unafanya kazi na mpiga picha, je, anaweza kuchukua picha baada ya mahojiano ili yule mhasiriwa asipigwe picha wakati anazungumzia matukio?
- Ikiwa unafanya kazi na mkalimani, je, ni mtu anayestakihi kwa kazi hiyo? Je, mkalimani anaelewa masuala hayo na je, amepewa maelezo kuhusu mahojiano ya aina hiyo?
- Je, mhasiriwa anajisikia nafuu kuzungumza na watu wa jinsia tofauti kwenye chumba cha mahojiano? Sio lazima kwamba wanawake wawahoji wanawake, au wanaume wawahoji wanaume, lakini hii ni jambo la kuzingatia.
- Hata kamaa anayehoji ni mwanamume wenye hisia nzuri, katika hali nyingi, mhasiriwa wa kike anaweza kujisikia salama akihojiwa na mwanamke mwenzake; ikiwa hiyo haiwezekani, inafaa kuwa na mwenzako wa kazi wa kike karibu. (Kuhoji watoto na vijana kuhusuunyanyasaji wa kijinsia kunahitaji utaalamu na bidi ya ziada. Kila mara jiulize ikiwa hii kweli ni jambo ambalo unapaswa kufanya).
- Ikiwezekana, muulize mhasiriwa ni nini anapendelea. Je! kuna mtu yeyote ambaye mhasiriwa anataka awe naye hapo, kama jamaa au rafiki wa kuaminika? Ikiwa unamhoji mtoto mdogo, mlezi wake anapaswa kuwepo.

Je, huyu mtu anafaa kuhojiwa?

Ambayo inayoweza kuwa Jiulize maswali haya rahisi:

- Je! mhasiriwa huyu yuko thabiti na katika hali inayofaa kuzungumza?
- Je! yuko katika hali inayofaa kuzungumza? Ni nini matarajio yake na je, ni matarajioyao ni yapi. Yanayowezekana?
- Je! unahitaji mahojiano haya? Je! yanaongeza chochote au unayo habari ya kutosha?

Mara nyingi, katika mazingira ya migogoro au ya baada ya vita, asasi zisizokuwa za serikali zinazofanya kazi nyanjani ndizo zinapatanisha wanahabari na huenda ndio wamekupangia kuzungumza na wahasiriwa wa ukatili wa kingono. Unaweza kujikuta kwamba asasi isiyokuwa ya serikali inaanda mtu yule yule au kikundi kidogo cha watu kwa ratiba finyo ya mahojiano na wanahabari. Kurudia hadithi tena na tena kwa muda mfupi inaweza kuwa ya kuchosha sana kwa mtu ambaye amepata kiwewe. Inaweza pia kuwa na athari za kisheria kwa mhasiriwa Ikiwa katika mahojiano tofauti mhasiriwa ameongea mambo yanakinzana kidogo, hili linaweza kudhoofisha nafasi zao za kutafuta suluhisho la kisheria baadaye [Tazama **#3**].

Kwa kuzingatia shinikizo la wakati ambalo wanahabari wanakumbwa nalo, ni rahisi kukubaliana na yale ambayo asasi zisizokuwa za serikali zitapendekeza. Lakini inafaa kuwa na mazungumzo kuhusu matakwa wanayowekewa wahasiriwa wakati unaowahoji. Unaweza kuwauliza ni mara ngapi wamehojiwa. Kuwa mbunifu – ikiwa unasafiri katika kundi la wanahabari, mnaweza kushirikiana katika utafiti wenu ili yule mhasiriwa aweze kuhadithia habari yake mara moja tu.

Akizungumza na *Columbia Journalism Review* mnamo mwaka 2019, Skye Wheeler wa shirika la Human Rights Watch alielezea juu ya vitendo visivyo vya maadili vya uanahabari na vya utafiti vilivyo fanyika kwa wahasiriwa wa ukatili wa kijinsia katika kambi za wakimbizi za Rohingya nchini Bangladesh:

> *“Bila shaka tunaweza kuangalia nyuma na kusema mambo hayakwenda sawa. Watu walihojiwa mara nyingi,” alisema Sky.* [a]

Zingatio la muhimu-ambayo inaweza kuwa ngumu kuhukumu ni kama mtu tayari anajisikia salama kisaikolojia kufanya mahojiano. Bado wanaweza kuwa wanahisi mfadhaiko ikiwa tukio hilo la kutisha lilitokea hivi karibuni. Kuna uwezekano mkubwa pia kuwa ukatili wa kijinsia haukutendeka bila matukio mengine – mhasiriwa anaweza kuwa amepitia aina nyingine za vurugu, amepoteza watu wa familia, au kuhamishwa kwa lazima. Kwa ufupi, je, wako katika hali ambayo wanaweza kuzungumza?

Inaweza kuwa shida kubwa kutathmini usalama wakihemko na wa kimwili kwa unayemhoji na pia kwako mwenyewe. Suluhisho mara nyingi ni kuwahusisha watu kikamilifu katika kupanga vile mahojiano yatakuwa, na kuwapa udhibiti juu ya jinsi yatakavyofanyika. Masuala haya mengi yanaingiliana na swali la idhini. Maelezo zaidi juu ya hilo tutayapata katika sehemu inayofuata.

Unyanyapaa na jinsi kuripoti inaweza kuharibika

Jiulize ikiwa kumhoji mtu flani kunahatarisha usalama wake na faragha. Katika jamii zingine, mtu akishukiwa kubakwa, inaweza kusababisha udhalilishaji, kutengwa na hata kusababisha vurugu zaidi.

Hapa kuna mfano kutoka Iraq kuonyesha jinsi mambo yanaweza kuharibika wakati wanahabari hawajafahamishwa kikamilifu kuhusu hali halisi.

Johanna Foster na Sherizaan Minwalla walichunguza mahojiano 26 ya maoni ya wanawake wa Yazidi juu ya hali na athari za kuripoti kuhusu wanawake na wasichana ambao walinusurika utekwaji, ubakaji, na usafirishaji haramu wa ISIS. Waliweka matokeo yao katika utafiti mwaka 2018. Hapa kuna dondoo muhimu:

> *“Kama wanawake wengi ulimwenguni, wanawake wa Yazidi wanakabiliwa na shida ya kawaida ya kijinsia ya kuulizwa kutanguliza mahitaji ya jamii kuliko yao wenyewe.*
>
> *“Hasa, walikuwa wanakabiliwa na uamuzi wa kujitolea kuhadithia matukio yao ya kufedhehesha kwa ulimwengu, licha ya hatari za kibinafsi, za mwili, sifa, na kihemko. Kwa kweli, wanawake wa Yazidi walihimizwa moja kwa moja kufanya hivyo na wanaume wa wa jamii yao bila hakikisho kwamba hawatanyiwa unyanyapaa kwa kupoteza heshima yao au kutendewa vibaya au kukataliwa na familia zao na jamii, haswa baada ya muda kupita.”.*

[a] Tazama: **https://www.cjr.org/analysis/rohingya-interviews.php**

Mmoja wa wanawake wa Yazidi aliyehojiwa alisema:

> *"Mwanzoni, niliporudi [kutoka ISIS], kamati ilikuja na kinasa sauti na kusema tutarekodi kisa chako. Niliwajibu kuwa 'hapana' kwa hivyo walikwenda kwa shemeji yangu na kumwambia, 'amekataa kuongea na sisi.'*
>
> *"Kuongeza kwenye suala la kulazimishwa, wanawake wa Yazidi waliishi katika kambi ambazo walizitegemea, na kwa hivyo walihisi kuwa na wajibu wa kufurahisha watoa huduma za kibinadamu, wafanyikazi wa kambi, na wanahabari ambao wote walitoa shinikizo kwa wahasiriwa kuhadithia visa vyao."*

Kwa sababu ya wanahabari kuangazia kisa hicho, kulikuwa na uwezekano wa kuongezeka kwa unyanyapaa wakati habari zilitolewa kwa msisimko kwa kutumia vichwa vya habari kama vile, "Mwanamke wa Yazidi aliyeshikiliwa kama mtumwa wa ngono kwa miezi mitatu na ISIS na kubakwa na genge azungumza kuhusu mateso ya kutisha"; "ISIS inauza wasichana watumwa wa ngono kwa 'bei kidogo kama pakiti ya sigara'" na "Wanawake wa Yazidi wanafanyiwa shunguli za matibabu ili "kurudisha ubikira" baada ya kubakwa na Daesh."[b]

Rasilimali Za Ziada: Usalama

Kuna miongozo anuwai ya kuweka salama kwenye kazi hatari zilizochapishwa na mashirika ya msaada wa vyombo vya habari na mashirika ya ulinzi. Tungependekeza kuanza na muhtasari uliotolewa na **CPJ** (Kamati ya Kulinda Waandishi wa Habari), Muungano wa ACOS (Utamaduni wa Usalama) na **Rory Peck Trust** (iliyoundwa kwa wafanyikazi huru), lakini kuna rasilimali zingine nyingi zinazofaa. (Mashirika yale yale pia yanaweza kushauri juu ya kupata mafunzo na aina zingine za msaada).

Salama na salama kutoka Jumuiya ya Doc imeundwa kwa watengenezaji wa filamu. Mbali na kutoa vidokezo juu ya usalama wa mwili, inatoa ushauri muhimu sana ambao utakuwa muhimu kwa mwandishi wa habari yeyote juu ya kuwalinda washiriki wa timu na wachangiaji kutoka vitisho vya usalama vya dijiti na dijiti - mambo mawili muhimu ambayo mara nyingi hupuuzwa. Mtandao wa Uandishi wa Habari za Uchunguzi wa Ulimwenguni pia unatoa **ukurasa huu wa kina wa rasilimali**.

Na ikiwa wewe ni mhariri au meneja, hakikisha uangalie zana ya tathmini ya **usalama ya ACOS kwa mashirika mapya na mwongozo** wa Kituo cha Dart cha kufanya kazi na **wafanyikazi huru walio wazi kwa kiwewe**. Frank Smyth kutoka CPJ ameandika ambayo **inazungumzia** hatari kwa waandishi wa habari wakati wa kufunika CRSV.

BONYEZA HAPA KUSHIRIKI SEHEMU HII:

[b] Johanna E. Foster na Sherizaan Minwalla, 'Sauti za Wanawake wa Yazidi: Maoni ya Mazoea ya Uandishi wa Habari katika Kuripoti juu ya dhuruma, Ukatili wa Kijinsia wa Isis,' Mkutano wa Kimataifa wa Mafunzo ya Wanawake 67 (2018): 53-64.

Tafadhali fikiria tu kuchapisha kurasa za nakala za greyscale

#3.

MASWALI MATATU YA MSINGI

JE! MHOJIWA WANGU ANAELEWA KIKAMILIFU WANACHOSAINI?

#3.

MASWALI MATATU YA MSINGI

JE! MHOJIWA WANGU ANAELEWA KIKAMILIFU WANACHOSAINI?

Haitoshi kwa mtu kusema ‘nakubali’ ili habari zao zichapishwe au picha zao kuchukuliwa. Idhini sio halisi kama haijaeleweka kikamilifu.

Kwa sababu tu mtu anakubali kuzungumza au anakubali picha yake kuchukuliwa haimaanishi kwamba anafahamu kikamilifu matokeo yake. Haitoshi kumwambia mtu unachotaka kufanya. Fanya la ziada ili kuhakikisha kuwa mhasiriwa anaelewa hatari na kumuonyesha kuwa ana chaguo halisi. Hasa, wanapaswa kufahamu:

- **Jinsi mchakato wa mahojiano au uchukuaji wa video utafanywa.**
- **Ni matukio na mambo gani unapanga kujadili.**
- **Nani ataweza kuona ripoti hio na kwa muda gani.**

Kupata idhini ni fursa na sio kama kikwazo ambacho kinaitaji kushinda. Ikiwa unayemhoji anafahamu hatari na anakubaliana nawe, utakuwa na mahojiano yenye nguvu.

Kiolezo cha kawaida cha uanahabari cha kupata idhini ya mhojiwa mara nyingi kinahusiana na kuhoji watu mashuhuri. Hawa mara nyingi ni watu wenye elimu ambao wanaelewa sheria zilizowekwa katika mchezo ambao wamezoea. Lengo kuu ni kumfikia na kumfanya mwanasiasa au mfanyabiashara aseme mengi iwezekanavyo, na inapendekezwa iwe hadharani na jina lao linawekwa wazi.

Ni wazi kuwa sampuli hii haifai wakati unafanya kazi na wachangiaji dhaifu, kwani usawa wa nguvu kati ya mhojiwa na mwanahabari umekuwa kinyume. Kwa kuongezea, wazo la kwanza katika hali ya ukatili wa kingono inapaswa kuwa ulinzi wa kutokujulikana kwa anayehojiwa. Hii inamaanisha kutokuwa na matarajio yoyote kwamba mhasiriwa ana jukumu la kuzungumza na umma.

Hili linafaa kuwa dhahiri. Kila mwanahabari anajua (au anapaswa) kujua hili. Lakini kwa upande mwingine, mtindo wa kisiasa umekita sana na bado unaweza kuwanasa wanahabari. Ikiwa unaripoti juu ya ukatili wa kingono kwenye migogoro, unahitaji kutulia na uhakikishe kuwa unaanzia mahali tofauti kwa kile kinachoitwa ‘idhini halisi’:

1. Kwanza, weka kando wazo kwamba idhini inahusu tu kumfikia mtu na kumfanya akubali mahojiano. Sio hivyo. Inahusu kuchunguza jinsi mtu anaweza kujenga msingi salama zaidi wa mahojiano ambao unaandamana na hatari kubwa. Ikiwa mtu atabadilisha mawazo yake na ikawa wazi kuwa hataki kuzungumza, basi chukulia hiyo kama inatosha. Kama ilivyo kwenye majaribio ya kuigiza, inamaanisha kuwa mtu huyo sio mwafaka kwa jukumu hili.

2. Pili, kupata idhini sio kitendo cha wakati mmoja au utaratibu wa kisheria ambao hufanyika mwanzoni tu mwa mazungumzo. Ni mchakato unaoendelea, na ni mjadala ambapo haki ya kuripoti kwa maelezo fulani – au hata kwenye mazungumzo yote yanaweza kubadilishwa zaidi ya mara moja.

Kamwe usishinikize au kumdanganya mtu kuongea kuhusu maisha ya kibinafsi kama ukatili wa kijinsia. Inapaswa kuwa ni chaguo huru na la kueleweka vizuri.

© Dart Centre Europe

Ni nani anaweza kutoa idhini?

Mtu pekee ambaye anaweza kutoa idhini ni yule unayemhoji. Ikiwa unayemhoji ni mtoto mdogo au mtu ambaye kwa namna fulani hana uwezo wa kutoa uamuzi kamili, unaweza kuhitaji pia idhini kutoka kwa mzazi au mlezi.

Lakini katika hali yoyote, **ikiwa huna idhini halisi kutoka kwa anayehojiwa – huna idhini tu**. Idhini kutoka kwa jamaa, wakili wa mtu, mpatanishi au mpatanishi kutoka kwa asasi isiyo ya serikali kuwa ni sawa kufanya mahojiano haikubaliki kama idhini. Maridhiano lazima yawe moja kwa moja na unayemhoji .

Ikiwa unafanya kazi na mkalimani, unahitaji kuhakikisha kuwa mazungumzo baina yake na mhojiwa, ni yale unadhani yanatakikana. Hii, kama mwandishi wa habari Jina Moore anaelezea, inaweza kuwa tatizo. Inaweza kuhitaji hatua za ziada. Huenda utahitaji kumwambia mkalimani yafuatayo:

> *“Samahani kujirudia, lakini nataka kuhakikisha lengo langu liko wazi: lengo langu ni hili. Niko hapa kwa sababu… ” Na mkalimani anaposema, “Nimeshamwuliza hivyo,” unajibu, “Ninathamini hilo, lakini sheria za kazi yangu zinahitaji kwamba nimuulize yeye mwenyewe moja kwa moja. Kwa hivyo, nakuomba kutafsiri tena ninachosema ili tuweze kuthibitisha hili tena…”*[a]

Tofauti za nguvu zinaweza kuwa si wazi na wahasiriwa wanaweza kuwa chini ya shinikizo la kuzungumza wakati sio kwa faida yao. Kama mwanahabari, una jukumu la kufuatilia kwa ndani kujua uwezekano wa kuathirika kabla ya kudhani kuwa mhasiriwa ana chaguo la kweli katika kutoa idhini.

Ikiwa mhojiwa amepitia shambulio hivi majuzi (kama vile dakika, masaa, na labda siku kadhaa) anaweza asiwe tayari kutoa idhini halisi. Kunaweza kuwa na njia ya kuripoti kile kilichotokea kwa kutumia habari za ziada kwa njia ambayo una hakika haitasababisha kutambuliwa kwa mhasiriwa. Lakini ni lazima ufahamu kuwa mtu aliye katika hali kama hiyo hayuko katika nafasi ya kufanya uamuzi kuhusu ikiwa atafutilia mbali haki yake ya kutokujulikana. Hiyo itahitaji muda zaidi baada ya shambulio. Hiyo itaitaji umbali zaidi kutoka eneo la shambulio.

Kufanya kazi na wakalimani

Ikiwa unafanya kazi katika eneo ambalo wewe si mwenyeji, utahitaji uhusiano wa wanahabari na wakalimani wenyeji ambao wanaweza kuzungumza lugha ya hapo na wanafahamu maeneo hayo. Lakini usidhanie kuwa lazima wanafahamu maswala ya kiwewe.

Unahitaji kuhakikisha kuwa kila mkalimani anaelewa kuwa:

- Mada inaweza kuwa ngumu kihemko. (Unapaswa pia kuangalia ili kuona ikiwa kuna hatari yoyote kwao au kwa familia zao).
- Haipaswi kushinikiza au kutoa vishawishi kwa wahojiwa kuongea.
- Je, idhini ya kueleweka na mahojiano kuhusu masuala ya kiwewe yanaendeshwa vipi. (Waonyeshe rasilimali kutoka kwa mwongozo huu).
- Wakati wa mahojiano, wanahabari hawapaswi kushinikiza wahasiriwa katika mambo ya huzuni au kutafuta habari isiyo ya manufaa.

Unapaswa kupanga kwa kina jinsi utakavyofanya mahojiano kabla ya wakati kadri uwezavyo na pia ikiwezekana kufanya mazoezi ya kile utakachofanya. Kuwa na ufahamu kamili juu ya hatari na kanuni za kitamaduni. Uliza mwelekezi wako pia kwa maoni kuhusu namna ya kuendesha mambo na ikiwa wanapata ugumu wa kukufanyia ukalimani. Pindi anakuwa na uaminifu kwako, kazi inakuwa bora zaidi. Unapashwa kuanglia jinsi wanavyoendelea ki binafsi na ikiwa kuna hatari yoyote kwao nafamilia zao.

[a] Katika kifungu cha Moore: **Mawazo Matano Juu ya Idhini ya Maana katika Uandishi wa Habari za Kiwewe**

Ni nini maana ya idhini halisi?

Kwa sababu tu mtu anakubali kuongea, haimaanishi kwamba anaelewa kikamilifu matokeo yake.

Inawezekana kuwa hawafahamu vizuri mchakato, nini utawauliza na jinsi hiyo inaweza kusababisha uchungu na pia nini kitatokea baada ya mahojiano. Cha muhimu ni kuzuia mshangao na chochote kinachoweza kusababisha madhara zaidi mbeleni. Angalia kuwa wewe na anayehojiwa mnaelewa vizuri kuhusu yafuatayo:

- Nini lengo la mazungumzo
- Nani atahusika
- Ikiwa kuna mambo ambayo hayawezi kuzungumziwa kabisa
- Nani ataona ripoti hiyo (na kwamba inawezekana kupatikana kupitia mtandao mahali popote ulimwenguni)
- Ikiwa ni video, itapatikana kwa muda gani na itasambazwa vipi
- Jinsi kutokujulikana kwao kutalindwa
- Ikiwa kuna uwezekano wa kutambuliwa na kufanyiwa madhara mtandaoni

Ikiwa unatumia picha, ni ada nzuri kumshirikisha mhojiwa katika uamuzi na kuwaonyesha nini watu wengine wataona juu ya maisha yao na jamii wanayoishi. Waandishi wa habari walioripoti juu ya ubakaji wa wanawake wa Yazidi na ISIS walidhani wanawake hao hawatajulikana kwa kuwapiga picha wakiwa wamefunikwa nyuso zao. Lakini wanawake wenyewe waliweza kujitambulisha kupitia macho yao na pia kwa sababu kila mmoja alikwa na mtandio unaombainisha. [tazama **#8**.]

Uzingativu zaidi utahitajika ikiwa, kwa mfano, masuala nyeti kama haya hayajafafanuliwa:

- Je! video au ripoti ya mwisho itakuwa na sauti za wahalifu, au vikundi vinavyowaunga mkono? Kugundua baada mambo yashafanyika inaweza kuhuzunisha sana. Aliyenusurika anaweza kuwa na ugumu mkubwa kuelewa kanuni ya 'haki ya kujibu' na jinsi mtu yeyote anaweza kuwapa wanyanyasaji nafasi ya kujibu. Ni bora kulielezea hili mapema.
- Je, kuna matarajio yaliyofichika ambayo hayajashughulikiwa? Je! mhojiwa wako anaamini kuwa kuzungumza na wewe kutaleta msaada wa moja kwa moja kwa jamii? Au ana matarajio kwako kuendelea kumpa msaada wa kisaikolojia au urafiki ambao huwezi kutimiza? [Kuna maelezo zaidi katika **#6**].
- Mara nyingi, wanahabari hawafikirii juu ya matokeo ya kisheria ya mazungumzo yao na wahasiriwa wa ukatili wa kijinsia kwenye migogoro. Ikiwa mhojiwa ana nia ya kutafuta haki kortini, basi kuzungumza na wanahabari kunaweza kudhoofisha kesi yake. Unapaswa pia kujua kwamba rekodi zako zote zinaweza kuchukuliwa kuwa ushahidi.

Mchakato wa kimahakama na hatari ya masimulizi yanayokinzana

Mchakato wa kisheria katika kutafuta haki kwa wahasiriwa wa vurugu wakati mwingine unaweza kuathiriwa na mahojiano mengi. Mwanahabari wa Colombia Jineth Bedoya anaelezea kama ifuatavyo:

> *Ni moja wapo ya shida kubwa tunayo katika visa vya ukatili wa kingono.*
>
> *Huko Colombia, sheria inasema kwamba mhasiriwa halazimiki kutoa ushuhuda wake juu ya tukio zaidi ya mara moja. Lakini, wengi wa wahasiriwa wanalazimika kutoa zaidi ya mara nne jambo ambalo linapelekea kutofautiana kwa ushuhuda ambayo mara nyingi husababisha kuzorota kwa michakato ya kimahakama. Athari inakuwa kubwa zaidi ikiwa mhasiriwa ametoa ushuhuda wake kwa vyombo vya habari.*
>
> *Kwa bahati mbaya, waandishi wa habari wanategemea kutokubaliana kwa ushuhuda ili kupata ile iliyo halisi jambo ambalo husababisha kufungwa kwa mchakato wa sheria.*
>
> *Vivyo hivyo, masimulizi ya kitendo cha jinai cha ukatili wa kingono, bila kesi, kinasababisha uwasilishaji wa hoja za utetezi kwa wahalifu, ambao mara nyingi hutegemea ushahidi wao juu ya" kukinzana kwa masimulizi"ambayo wahasiriwa wameongea katika mahojiano na chombo cha habari. Waamuzi hawazingatii mazingira ya njia, wakati, na mahali ambapo ushuhuda wa mhasiriwa hutolewa hadharani. Na ni wazi kuwa athari ya kisa ni tofauti katika mahojiano na mwandishi wa habari kuliko na mwanasaikolojia au mtaalamu wa afya.*

Jineth Bedoya Lima, ambaye alichangia katika utafiti wetu, alitekwa nyara mara mbili huko Colombia mnamo Mei 2000 na Agosti 2003. Mnamo 2001, alipewa Tuzo ya Courage In Journalism Award kutoka kwa shirika la **International Women's Media Foundation**. Pia alishinda tuzo ya 'Golden Pen of Freedom' kutoka **World Association of Newspapers and News Publishers** mnamo 2020.

Rasilimali za ziada

Jina Moore, mwandishi wa habari wa Amerika anayefanya kazi Afrika Mashariki, ameandika makala mawili muhimu yanayoelezea maswala ya idhini kwa undani zaidi: Mtego wa **Ponografia katika** jarida la Columbia Journalism Review na pia: **Mawazo matano juu ya idhini ya maana katika Uandishi wa Habari za Kiwewe**.

BONYEZA HAPA KUSHIRIKI SEHEMU HII:

Tafadhali fikiria tu kuchapisha kurasa za nakala za greyscale

#4.

MAZOEA MATATU MUHIMU KWA MAHOJIANO SALAMA

WAPE WAATHIRIKA KUZUNGUMZA KWA NJIA WANAYOTAKA NA KWA WAKATI WANAOTAKA

#4.

MAZOEA MATATU MUHIMU KWA MAHOJIANO SALAMA

WAPE WAATHIRIKA KUZUNGUMZA KWA NJIA WANAYOTAKA NA KWA WAKATI WANAOTAKA

Wakati wa ukatili wa kijinsia, wahalifu huchukulia watu kama vitu - sio kama watu ambao wana uwezo wowote juu ya kile wanatendewa. Je! unaweza kubadilisha mtizamo huo na kuwapa wahojiwa nafasi ya kujieleza?

Uhitaji wa kuwatendea watu walio katika mazingira magumu kwa uzingativu, heshima na hadhi inapaswa kuwa kitu cha wazi. Lakini hiyo inahusisha nini katika njia inayofaa?

Kama mwanahabari anayehoji mhasiriwa, uko katika nafasi ya nguvu - hata kama huhisi hivyo. Maswala yatakuwa kuhusu uaminifu na usalama wa kihisia. Kwa hivyo, ni muhimu usifanye chochote ambacho kinaweza kumkumbusha mhasiriwa ukatili uliotekea hata kwa njia ndogo kama vile kuwaharakisha au kushinikiza majibu. Hii inaweza kuwa rahisi kupuuza wakati ni mfupi ukiwa katika eneo lenye hatari.

Kwa hivyo, panga wakati wa kutosha wa mazungumzo na hakikisha kwamba mtu anayehojiwa anajua haya:

- **Hawajibiki kujibu maswali yoyote ambayo hangependa kusema.**
- **Ni sawa kusimisha mahojiano wakati wowote.**
- **Kwamba hutachapisha maelezo yoyote ambayo mhasiriwa anakuomba usichapishe.**

Muone anayehojiwa kama mtu kwanza - na pili tu kama chanzo na nyenzo ya adithi yako.

Mahojiano ya vyombo vya habari yanaweza kusababisha madhara kwa wahasirika ikiwa ni mahojiano hayo yanafanywa kwa njia ya ukandamizi au bila kuzingatia usalama. Sehemu hii inazungumzia misingi ya mahojiano yanayofaa; namba **#5** inaangalia kwa undani zaidi athari maalum za kiwewe na changamoto zake wakati wa kufanya kazi na wahasiriwa.

Mara nyingi, wanahabari wana wasiwasi kuwa kitendo cha kuzungumza juu ya visa vya kuumiza na vurugu kama vile ukatili wa kijinsia au mateso inaweza kusababisha madhara kwa anayehojiwa. Wanahabari wanaweza kuogopa kuwa wanawakumbusha wahasiriwa mambo ambayo ni afadhali kunyamaza. Au wanaweza kulinganisha shida ambayo mtu hupata wakati wa kusimulia hadithi yao na kusababisha madhara mapya.

Wataalam wengi wanaoshughulikia mambo ya kiwewe wanaofanya kazi na wahasiriwa wa ukatili wa kijinsia hawaoni kwamba kitendo cha kuongea kwa kivyake ndio chanzo cha hatari. Inahusiana zaidi na jinsi mhojiwa anavyojisikia salama wakati wa mazungumzo, na namna gani ana uwezo juu ya kile kinachozungumzwa, na pia jinsi kisa chake kitachapishwa baadaye [angalia **#7** na **#8**]. Madhara yanaweza kutokea wakati watu wanahisi kuhukumiwa, kutosikilizwa, au kuhisi kuwa wanatumiwa kwa malengo mengine kama vile kupata habari ya kuuzika. Katika mahojiano ya masuala yanayohusiana na kiwewe, uaminifu ni kitu laini ambacho kinaharibika kwa urahisi.

Kuna wakati mwingine haitoshi kufikiria kwamba kuzungumza peke yake haitaleta madhara. Kwa mfano, ikiwa mtu amepitia jambo la kufedhehesha sana wakati wa zamani na kusahau matukio hayo na hawajawahi chunguzwa hapo awali – kama unyanyasaji wa kijinsia wa watoto, basi kuongea kuhusu tukio hilo inaweza kuamsha hisia mbaya na kuleta hatari tofauti. Kwa ujumla, kuwa mwangalifu usiwape habari za kushangaza na zisiyotarajiwa.

Jinsi ya kufanya mchakato kuwa wa kushirikiana zaidi kuliko kuonekana kutafuta habari tu

Watu waliopitia ukatili wa kijinsia huhisi kama wamepoteza udhibiti wao- kitu ambacho kiliwapata ambacho hawakuwa na uwezo wa kuzuia. Njia moja ya kukabiliana na jambo hili ni kumpa mtu udhibiti ambao unaweza kutumia kama mwanahabari na kumshirikisha mhojiwa wako katika maamuzi juu ya mchakato huu. Hata mamuzi madogo yanaweza kuleta mabadiliko makubwa.

Kabla ya kuanza mazungumzo unapaswa:

- kukiri kuwa wakati mwingine inaweza kuwa vigumu kuzungumza
- wahusishe kikamilifu katika uamuzi kuhusu wapi wangependa kuhojiwa
- ni saa gani ya siku ambayo ingewafaa zaidi – ni lini wangeweza kuwa na nguvu zaidi kwa mahojiano na wangependa kuongea kwa muda ga ni?
- Je, kuna mtu yeyote ambaye angependa kuwa pamoja nae kwenye chumba kama vile rafiki au jamaa?
- muulize ikiwa kuna kitu chochote ambacho hangependa wasizungumzie
- na uwahakikishie kuwa sio lazima kujibu kile ambacho hawataki

Ni ada nzuri kuuliza watu kabla ya kuanza mazungumzo jinsi wewe kama mhojiwa utakavyotambua vipi hawataki kuongea zaidi na wanataka kusimamisha mazungumzo. Katika hali ya kuhadithia kisa watu wanaweza kujisahau. Kwa kuongezea, wengi wetu tunakuwa na hamu kubwa ya kuendelea kuongea ili kumpendeza mtu anayeuliza maswali. Wanaweza kuwa sio wazuri sana kuashiria wakati wamechoka au wakati mazungumzo yameingia katika mada ambayo hawangependa kuzungumzia na kuwafanya wahisi vibaya. Kuangazia hili kabla ya mahojiano kuanza – na labda kukubaliana kwa ishara maalum – hufanya kupendekeza mapumziko au kubadilisha mada iwe rahisi bila usumbufu.

Makubaliano kuhusu maneno ya kutumia

Sehemu ya **#7** inazungumza zaidi juu ya chaguzi za lugha wakati wa kuchapishwa. Wakati wa mahojiano yenyewe, hakikisha kuwa unatumia maneno ambayo mhojiwa anaridhika nayo. Huenda kutumia misamiati inayotumiwa na wenyeji isiwe na manufaa. Kuna sheria zilizo wazi. Kwa mfano, haifai kamwe kumuita mhalifu kama mpenzi wa mtu.

Watu wengi ambao wamepitia ukatili wa kijinsia wanajielezea kama ‘manusura’; lakini wengine wanaweza kuhisi kuwa “mhasiriwa” ni neno sahihi zaidi; na wengine wangependa kuepuka yote mawili. Ikiwa una shaka juu ya maneno gani ya kutumia, muulize mhojiwa wako nini angependelea. Kwa ujumla, ni muhimukila wakati kuheshimu jinsi watu wanajitambua.

Nguvu ya kusikiliza

Wakati watu wanaamini wanasikilizwa, wanajisikia salama zaidi na wanaweza kuongea kwa ufanisi zaidi. Kujua jinsi ya kusikiliza vizuri labda ni ujuzi muhimu zaidi ambaambao mwanhabari anahitaji wakati wa mazungumzo na mhasiriwa. Hii ni pamoja na kutoa nafasi kwa mhojiwa na kuuliza maswali rahisi na yaliyo wazi ambayo humpa mtu chaguo ya jinsi wanataka kujibu lakini sio wazi sana kiasi kwamba inawalemea kujibu.

Kumbuka kwamba kama ilivyojadiliwa katika sehemu ya **#2**, kutafuta idhini ni mchakato unaoendelea na sio tukio la wakati mmoja. Na kwa hivyo unaweza kutaka kutanguliza swali, Je! *ni sawa kuuliza kuhusu* ... (mada maalum au tukio). Kisha, mpe mhojiwa nafasi ya kujibu kwa uhuru.

Katy Robjant ambaye anafanya kazi na wahasiriwa wa ukatili wa kijinsia katika migogoro nchini Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo na maeneo mengine ana ushauri huu maalum kwa waandishi wa habari:

> *Badala ya kuuliza maswali ya wazi kuhusu matukio kwa ujumla, hakikisha na mhojiwa wako kwamba kuna jambo maalum unatarajia kuzungumzia. Kisha muulize akuambie kadiri awezavyo kuhusu tukio au mada hiyo. Baada ya kukupa habari zote ambazo angependa kuzungumzia, kazi yako inabaki kuuliza maswali*

muhimu. Hii ni njia moja ya kuzuia kumlazimisha mhojiwa wako kuzungumza mambo ambayo hataki kusema au kufikiria.[a]

Ushauri kuhusu usikilizaji mzuri ni pamoja na:

- kuruhusu ukimya na kuwapa watu nafasi ya kufikiria
- kutumia maneno au, ikiwa unarekodi, kutumia alama za ishara kuonyesha kuwa bado unamsikiza
- kuuliza ili kuhakikisha kuwa umeelewa vidokezo muhimu
- Kujua jinsi ya kukaa na usumbufu wako mwenyewe na kutoruhusu kuchukua mwelekeo mbali na aliyehojiwa.

Jaribu kuepuka:

- kumaliza sentensi za mhojiwa au kukata mawazo kwa ghafla (isipokuwa kama anajisahau katika kumbukumbu – angalia sehemu ya **#5**).
- kuonyesha ishara ya kumhukumu mhojiwa, kwa mfano kwa kuonyesha uso wa kutisha wakati mtu anasimulia jambo ambalo linaweza kutisha (kuonyesha wasiwasi au huruma ni sawa.)
- maswali kuhusu maelezo ya ndani au ya mwili
- Kumwambia mhasiriwa kuwa unajua jinsi anavyohisi ((inawezekana asikuamini kwa hili)

Unapaswa pia kuwa mwangalifu kuhusu kumwambia yule unamhoji kuwa umepetia mambo kama hayo au kuongea sana kuhusu historia yako. Katika hali zingine, hii inaweza kusaidia kujenga uaminifu na kukuza mazungumzo; kwa upande mwingine, inaweza kuondoa mwelekeo mbali na anayehojiwa na kumuacha akihisi kuwa matukio yao yanapuuzwa. (Hitaji la kudumisha mipaka ya kiafya limejadiliwa zaidi katika kifungu cha namba **#6**).

Mpangilio wa wakati na kutamatisha vizuri

Kichwa cha sehemu hii, *Kuruhusu wahasiriwa nafasi ya kuongea kwa njia na kwa wakati wanaoridhia* haimaanishi kwamba huna nafasi yoyote kwenye mpangilio wa wakati. Wakati watu ni wanyonge, wananufaika na mazungumzo yakiwa na miongozo. Na kama ilivyoelezwa hapo juu, unahitaji kuangalia viwango vyao vya kuendelea kuzingatia (Ikiwa uko katika eneo hilo kwa muda mfupi unaweza kupendekeza kurudi mara nyingine ili kuendelea na mazungumzo.)

Madaktari wengine huzungumza juu ya sheria ya theluthi tatu. Kuwa katika theluthi ya kwanza ya mazungumzo yanapaswa kuzingatia wakati na matukio ambayo mhojiwa alihisi salama; sehemu ya pili ni kwenye mazungumzo magumu zaidi, kwa mfano matukio yanayoleta kiwewe; na sehemu ya mwisho ni kuhusu maisha ya sasa na ya baadaye – chochote kinachosaidia mhasiriwa kurudi hali ya sasa. Sio vizuri kumuacha mtu mwishoni mwa mahojiano akiwa bado amezama kabisa katika yale mabaya yaliyompata.

Jaribu kumaliza kwa njia nzuri lakini usilazimishe na kujifanya kuwa mambo ni bora kuliko yalivyo. Unaweza kumuuliza mhojiwa ni nini ameona ni muhimu katika kupambana na hali hii na nini angependekeza kwa wengine. Si rahisi kila wakati kupata namna nzuri ya kumaliza mahojiano. Kwa uchache, unaweza kumuuliza mhojiwa nini watafanya muda uliobaki siku hio. Kumbuka, kuwashukuru wahusika na kuhakikisha unatimiza ahadi zozote unazotoa kama vile, mawasiliano ya baadaye, kutuma habari kuhusu makala na kadhalika.

BONYEZA HAPA KUSHIRIKI SEHEMU HII:

[a] Tazama: **https://dartcenter.org/resources/reporting-refugees-tips-covering-crisis**

Tafadhali fikiria tu kuchapisha kurasa za nakala za greyscale

#5.

MAZOEA MATATU MUHIMU KWA MAHOJIANO SALAMA

KUELEWA ATHARI ZA KUENDELEA ZA KIWEWE KWENYE KUMBUKUMBU NA HISIA ZA USALAMA

MAZOEA MATATU MUHIMU KWA MAHOJIANO SALAMA

#5. KUELEWA ATHARI ZA KUENDELEA ZA KIWEWE KWENYE KUMBUKUMBU NA HISIA ZA USALAMA

Ujuzi wa kimsingi kuhusu kiwewe yanaweza kukusaidia kuendesha shughuli ngumu ya mahojiano na kuepuka makosa ya kuripoti.

Wahasiriwa wanaweza kukasirika wanapohadithia tena tukio mbaya. Kuwa katika huzuni haimaanishi wahasiriwa hawako kwenye nafasi nzuri ya kuzungumza. Lakini athari zingine zinaweza kuonyesha kuwa wahasiriwa hawajisikii salama tena kuendelea na mazungumzo. Wanaweza kujitenga, kutafuta mlango, au kupata athari za mwili sawa na zile walizopata wakati wa shambulio.

Kiwewe ni *tukio gumu kimada, kisaikolojia na kijamii*. Huzuni sio jambo moja tu - ni mchanganyiko wa vitu tofauti. Kama mtaalamu wa uandishi habari hauitaji kujua sayansi ya ubongo lakini unahitaji kufahamu mambo ya kimsingi ambayo yanaweza kukusaidia kufanya maamuzi bora kuhusu yafuatayo:

- **Jinsi mhojiwa wako anavyoendelea na ni lini anaweza kuhitaji muda wa kupumzika kuongea.**
- **Jinsi ya kujiepusha na aina ya maswali ambayo inakufanya uonekane kama mchunguzi jambo ambalo linaweza kumfanya awe na hisia ngumu kama vile ya hatia na aibu.**
- **Ni kiasi gani utategemea usahihi wa kumbukumbu ya mtu kwa tukio la kutisha na kwanini haifai kuuliza maswali magumu kwa lile mhasiriwa amesahau.**

Ubakaji ni moja wapo ya matukio mabaya sana ya kufedhehesha ambao mtu anaweza kupitia. Kuna sababu nyingi ambazo wahasiriwa wanaweza kupata ugumu katika kuelezea matukio yaliyowakumba. Aibu na hofu ya jinsi wengine wanavyoitikia inaweza kuwa sababu kubwa katika kufanya mhasiriwa asiweze kuzungumza. Na kuzungumza kuhusu kiwewe kunaweza kuleta hisia kali ambazo wahasiriwa wanaweza kuhisi uchungu mwingi na ni ya kuchosha kuzungumzia. Wakati mwingine ukimya ndio jibu bora.

Lakini mara nyingine inawez kuwa vigumu kuzungumza kwa sababu tofauti zinazohusiana na jinsi kumbukumbu ya mwanadamu inavyofanya kazi katika hali za kiwewe.

Wakati tunashambuliwa tunaingia kwenye hali ya kuondoka kwenye hatari. Kumbukumbu bado zimesajiliwa – mara nyingi kwa undani kabisa – lakini ubongo hauchuji na kurekodi kulingana na mpango wake wa kawaida (badala yake, inaipakipaumbele mifumo ya msingi zaidi ya kutoka hatarini). Kwa hivyo, ni kawaida kwa watu ambao wamenyanyaswa kingono kuwa na shida na kumbukumbu zao kwa zimechanganyika na kukosa mpangilio. Kunaweza kuwa na mapungufu au kutofautiana katika mpangilio ambao wana shida kukumbuka. Mambo mengine yanaweza kurudi na nguvu fulani za kipekee; mengine yanaweza kusahaulishwa au hata bila kukumbukwa.[a]

Kama mwanahabari, hii inamaanisha:

- Haupaswi kutarajia mhasiriwa kukupa masimulizi madhubuti kabisa au ya kimantiki ya kile kilichotokea. Kutofautiana sio ushahidi wa nia yoyote ya kudanganya.

[a] Kwa utangulizi muhimu wa athari ya kiwewe kwenye kumbukumbu kwa waathirika wa unyanyasaji wa kijinsia ona: G. Smith na S. Heke, ‘Kutoka Ripoti kwenda Mahakamani: Saikolojia, Jeraha, na Sheria’ (2010), inapatikana **hapa**.

- Sio haki kutarajia unayemhoji arekebishe tofauti ya masimulizi yeye mwenyewe – huenda hawezi kufanya hivyo. Ikiwa ni muhimu kupata msururu wa hakika, tafuta njia zingine za kuthibitisha matukio.
- Kurudi nyuma na kuuliza swali rahisi la kufafanua ni sawa ikiwa limeulizwa kwa njia nyepesi. Lakini ikiwa unapata pengo au kikwazo katika kumbukumbu ya mhasiriwa, usimsukume sana ili kutaka habari zaidi. Hiyo inaweza kurudisha kumbukumbu ya matukio kwa njia ambayo inakumlemea mhasiriwa[tazama sanduku hapa chini].
- Watu wengine unaofanya nao kazi, kwa mfano wahariri na wachunguzi wa ukweli, wanaitaji pia kujua hii.

Kujibu masuala ya huzuni

Dhiki haionyeshi lazma kwa njia ambayo tungetarajia. Unaweza kupata watu ambao wanaonekana kuwa wasio na hisia na wanazungumza juu ya mambo magumu kabisa bila shida au wengine wanatumia kicheko kama namna ya kutoa shida; jambo ambalo linaweza kuwa si la kawaida kwako. Hizi zote ni athari za kawaida ambazo zimethibitishwa ambazo watu binafsi wanapitia baada ya kukumbwa na kiwewe. Mtendee kila mtu unayekutana naye kwa uwazi na uwe mwangalifu usionyeshe kwamba unafikiri kuna njia sahihi ya kujibu.

Wakati watu wanazungumza juu ya matukio, mhasiriwa anaweza kupata hisia na athari za mwili ambazo walizipata wakati walishambuliwa. Athari hizi zinaweza kuwa nyepesi na isiyoonekana sana au hadi kushinikiza watu wengine wasiweze kuvumilia hisia hizo tena.

Ikiwa mtu ana athari kali – kwa mfano, kukasirika haraka, kuanza kulia nk – fanya mambo taratibu kabla ya kukimbilia kufanya chochote. Kuzima kamera kwa haraka au kuvunja mahojiano kunaweza kumuaibisha mhasiriwa bila kukusudia kwani anaweza kuhisi kuwa amekosea kuwa na hisia kama hizo. Kuwa mwangalifu pia na mguso wa mwili: hiyo inaweza kuwa ya kutishia na kuleta wasiwasi, haswa ikiwa haikutarajiwa. Badala yake, unaweza:

- Kuonyesha utulivu.
- Sema jinsi unasikitika kwamba jambo hili lilitokea kwake.
- Mkumbushe mhasiriwa kuwa ako salama hapa chumbani – na kwamba kitendo kile hakifanyiki sasa.
- Muulize ni nini kinachoweza kumsaidia kwa wakati huu. *Je, angependa mahojiano yasimamishwe kwa muda? Je, kawaida hufanya nini anapohisi hivi?*

Wakati mtu anapotelea kwenye kumbukumbu

Kujitenga ni athari ya kawaida ya kujitoa hatarini ambayo hujileta wakati wa vurugu za kijinsia. Wakati hali ni ya kulemea na hakuna njia halisi ya kutoroka, ubongo unaweza kwa ghafla kufanya akili ianze kufikiria kana kwamba shambulio halifanyiki muda huo.

Kuhadithia tena tukio kunaweza kumkumbusha mhasiriwa kama kwamba vurugu inafanyika tena sasa. Sio rahisi kila wakati kusema wakati mtu hajiskii salama na anaelekea kujitenga. Lakini mhasiriwa anaweza kuanza kuonyesha dalili hizi:

- Kukosa mazingatio, kuonekana mwenye usingizi, au kuacha kujibu maswali.
- Kulalamika kwa kuhisi joto au jasho la ghafla.
- Kulalamika kwa maumivu ya kichwa au maumivu ya mwili.
- Kuangalia chumbani ili kutafuta njia ya kutoka.

Katy Robjant, daktari wa saikolojia ambaye hufanya kazi na wakimbizi na wahasiriwa wa ukatili wa kijinsia katika migogoro nchini DRCongo na mahali pengine, hutoa ushauri huu kwa waandishi wa habari kuhusu nini cha

kufanya ikiwa hii itatokea:

> *Fanya vitendo vyako viwe vya kutabirika… Ni bora kuomba ruhusa au kumjulisha mtu huyo nini unataka kufanya… Jambo bora la kufanya ni kujaribu kumrudisha hali ya kawaida. Endelea kuongea. Uliza kuhusu mambo yanayotendeka kwa sawa kama vile, "Unaweza kuniambia uko wapi? Je, unaweza kuelezea chumba hiki kinakaaje? " Aina hizo za maswali zitasaidia zaidi kuliko maswali ya jumla kama, "Je, uko sawa?"[b]*

Aibu na kuaminika

Ni muhimu kuelewa jinsi ilivyo rahisi kwa hisia kali za aibu na hatia huibuka katika mazungumzo juu ya ukatili wa kijinsia. Hii inaweza kutokea ghafla na kuonekana kuwa hailingani na kile kinachojadiliwa wakati huo. Sio vigumu kuona mhasiriwa anajilaumu kwa mambo yaliyompata na ambayo labda sio kwa kosa lake.

Na hii sio tu kwa ukatili wa kijinsia – wahasiriwa wa ubakaji mara nyingi inabidi wakubali kuwa watu wa familia yao na katika jamii wanakosa kuwaamini na kupuzilia mbali kile wahasiriwa walifanyiwa au pia kuwalaumu kwa nia moja ama nyingine.

Na kwa hivyo kuwa mwangalifu sana na uepuke kutumia lugha yoyote ambayo inaweza kumaanisha kuwa humuamini mhasiriwa au kwamba analawama kwa njia yoyote kwa yale yaliyowapata. Kwa sababu hii, maswali kama *"Kwanini"* yanaweza kuwa hatari. Wachunguzi wanapenda kutumia maswali kama haya kwa sababu ni ngumu kujibu na inaleta hisia ya hatia. Kwa mfano, kumuuliza mhasiriwa *"Kwanini ulikuwa hapo wakati huo?"* inafanya ahisi kwamba hakupaswa kuwa hapo.

Aina ya maswali ambazo hutafuta habari juu ya hisia, kama vile *"Ulijisikiaje wakati…?"* pia ni bora kuepukwa kwani yanaweza kufufua na kuongeza uchungu wa hisia kali.

Na kama ilivyojadiliwa hapo awali, epuka kuuliza maswali ya kiuchunguzi ambayo yanataka maelezo ya kibinafsi au ya mwili ya kile kilichotokea.

Ikiwa mhasiriwa anaamini jambo ambalo unajua sio kweli au haukubaliani nalo na unataka kumuuliza, jiulize ikiwa wewe ndiye mtu sahihi wa kufanya hivyo na jambo hilo litasaidia nini. (Wakati mwingine watu hushikilia imani fulani kama ngao ya mambo ya yaliyomtokea ambayo huhisi ni mazito sana kuweza kuyakubali).

BONYEZA HAPA KUSHIRIKI SEHEMU HII:

[b] Tazama: https://dartcenter.org/resources/reporting-refugees-tips-covering-crisis.

Tafadhali fikiria tu kuchapisha kurasa za nakala za greyscale

MAZOEA MATATU MUHIMU KWA MAHOJIANO SALAMA

FAHAMU JINSI HISIA ZAKO PIA ZINAHUSIANA NA MASUALA HAYA

#6.

MAZOEA MATATU MUHIMU KWA MAHOJIANO SALAMA

FAHAMU JINSI HISIA ZAKO PIA ZINAHUSIANA NA MASUALA HAYA

#6.

Kutangamana na matukio ya ukatili inaweza kuleta athari kwa wanahabari. Kujitunza ni jukumu lako mwenyewe - na kwa wale unawahoji

Kuripoti kuhusu ukatili wa kijinsia kunachosha kihisia ambayo huja na hatari za kibinafsi kwa wanahabari wanaofanya kazi katika mazingira hatari na yasiyokuwa na utulivu. Unaweza kuwa na mwelekeo wa kuupuza huzuni yako mwenyewe kwa sababu unahisi ni kidogo ikilinganishwa na kile wahasiriwa wanapitia. Hata hivyo, unapaswa kufahamu kuwa athari hizo za zinaweza kuongezeka baada ya muda na kuleta athari mbaya zaidi na kuathiri jinsi unavyohusiana na wenzako na wahasiriwa.

Kuingizwa kwa hali ambayo unampa mhasiriwa ahadi za msaada wa kihemko na za kimada ambazo haziwezi kutimizwa ni mfano mmoja wa kile kinachoweza kutokea wakati mwanahabari au mtengenezaji wa filamu analemewa na habari anazokumbana nazo. Kwa hivyo, zungumza na wengine, fuata mkakati wa kujitunza na uwe wazi juu ya kile unaweza na usichoweza kufanya katika kuwasaidia wengine.

Audre Lourde, mwanaharakati mweusi wa Amerika wa haki za raia, aliwahi kuandika:

> *Kujitunza sio anasa. Ni kujihifadhi…*

Kuripoti kuhusu ukatili wa kijinsia inahusisha kukabiliana na baadhi ya mambo ya kusumbua ambayo watu wanaweza kuwatendea wengine. Wanahabari hawatumii nafasi kubwa kujadili umuhimu wa kujitunza na uelewa wa kiwewe, ingawa ni mada kuu kwa madaktari na wengine wanaofanya kazi na masulala yanayohusiana na kiwewe.

Ukweli ni kwamba waandishi wa habari na watengenezaji wa filamu ambao huchagua kuripoti matukio haya huwa ni watu wenye motisha na wenye ujasiri. Hata hivyo, kazi aina hii ina hatari kubwa za uchovu, unyogovu, matumizi mabaya ya dawa za kulevya na mafadhaiko ya baada ya matukio ya kiwewe. Hata pale ambapo athari ni ndogo, ugumu ambao tunaweza kuwa nao katika kutafakari yaliyomo kwenye kazi inayohusiana na kiwewe inaweza kuwa na athari kwa wahasiriwa ambao tayari wako hatarini.

Huruma kama daraja la njia mbili

Uwezo wa mahusiano ya huruma na wengine na kupima kwanini wako na kihemko ni sifa muhimu ya kuwa muhoji mzuri. Ni kwa njia ya huruma ndio tunaunda nafasi ambazo watu wanahisi kueleweka na salama ili waweze kuhadithia matukio yao. Pia ni njia ya kuelewa ni nini muhimu katika kisa kupitia kujaribu kuona vitu kutoka kwa hali ya mtu mwingine.

[a] A research breakdown can be found at **https://dartcenter.org/content/covering-trauma-impact-on-journalists**.

Huruma hufungua uhusiano wa njia mbili kati ya mhoji na anayehojiwa na kuunda njia ya mambo kufanyika. Kama mwenye kuhoji, unaweza kujipata wakati mwingine ukichukua hisia za watu wengine bila kujua kinachotokea. Hisia kali kama aibu, kukosa msaada na uoga zinaweza kuambukiza kwa njia ambazo zinaweza kuwa njia isiyo wazi na ngumu kujua. Sio ajabu waandishi wa habari kujisikia na huzuni baada ya kufanya mahojiano ya kufedhehesha.

Vivyo hivyo, kusikia au kusoma matukio yanayorudiwa ya jinsi watu walivyoshambuliwa au kuteswa, kunaweza kusababisha mawazo na picha zinazokuja kwa fikra zako kwa nyakati zisizotarajiwa. Athari hizi kawaida ni za muda mfupi na zisizo na nguvu – na kwa kiwango fulani – lakini zinaweza kuwa na athari za kiafya ikiwa zitaongezeka kwa muda na kukithiri. Jambo hili linaitwa kiwewe ambacho si cha moja kwa moja pamoja na athari zinazoweza kutokea kutokana na kupitia moja kwa moja au kushuhudia vurugu.

Kuvutwa kwenye shida za watu wengine

Kuna nadharia kuwa wanahabari hawapaswi kamwe kuhusika kihemko. Ingawa hilo ni wazo la kufurahisha, sio jinsi mambo yanavyofanya kazi. Kuna uwezekano mkubwa kwamba wakati fulani utahisi hali ya kujali na hamu ya kusaidia. Ikiwa hilo litatokea, ni muhimu kuwa wazi juu ya mipaka yako kama mwanahabari kuhusu nini unaweza na huwezi kufanya katika kutoa msaada. Mipaka inaweza kuwa si wazi kwa njia kadhaa zisizosaidia kama vile:

- Unaweza kuhisi kuwa wewe sio kama mtaalamu bali muelekeo wa kuwa kama rafiki. Hisia ya kusaidia inaeleweka lakini haitimiziki ikiwa hauko katika nafasi ya kutimiza jukumu hilo. Hatari iko katika kujenga matumaini ya uwongo ya kuendelea na msaada wa kihemko na usaidizi wa kimada ambao mtu hana uwezo wa kutoa. Kumbuka, ni rahisi kujenga matumaini ya watu bila kujua: na kwenye kiwewe, hisia kali kama kushikamana na usaliti yanaibuka. Inawezekana kabisa kuwa mwanadamu kamili na wa maadili bila kuwa kama rafiki.
- Unaweza kuwa umepitia ukatili wa kijinsia. Hii inaweza kukupa ufahamu muhimu lakini inaweza pia kukuweka mahali ambapo mambo uliyoyapitia yanaingiliana na yule unamhoji, jambo ambalo linaweza kukupelekea kutomuona mhasiriwa kama mtu tofauti, wa kipekee.
- Unaweza kuanguka katika mtego wa kutaka kuamini kuwa mahojiano hayo yatakuwa ya kimatibabu na ya kumsaidia mhasiriwa kwa njia fulani. Ni kweli kwamba wahasiriwa mara nyingi hupata faraja katika kuongea, na kuzungumza kunaweza kumsaidia mtu kujitoa katika mawazo ya kutatanisha na ya uchungu. Lakini wewe kama mwanahabari huna njia ya kumhakikishia jambo hili. Katika jamii ya misaada, hii inaitwa *hisia ya mkombozi*, na inaweza kuleta matatizo makubwa.

Ugumu katika kuelewa athari za kibinafsi zinaweza kuondoa mahojiano kwenye mkondo wake. Kwa mfano, ikiwa tunakasirishwa na watu kwa kutofanya zaidi kujisaidia, au ikiwa tunaanza kuorodhesha mateso ya watu wengine na yale ambayo ni juu zaidi kuonekana kuwa yanastahili kuzingatiwa.

Nini cha kufanya kuhusu haya yote?

Suluhisho sio kukata tamaa au hisia za kufanya hio kazi. Kuzuia majibu ya kibinafsi hakutasaidia. Na zaidi ya hayo, zote mbili ni sehemu za ushujaa. Badala yake, chukulia huruma kama misuli inayofaidika na kupumzika kimkakati. Kuchukua muda mbali na kazi huleta mtazamo, na nafasi ya kujiburudisha na kujitenga na matukio yenye kuumiza. Kukuwa na mitizamo mizuri katika maisha ni muhimu. Hapa kuna mambo ambayo yanaweza kusaidia:

- **Kuwa na shughuli ambazo zinakuruhusu kujiweka mbali na makala yenye kuogofya** (na chochote kinachokukumbusha kazi kwa ujumla). Mambo ya kuptisha muda kama kusoma kitabu, nk, chochote ambacho kinatoa fikra zako kwenye mada. Uzingativu ni jambo jingine linalosaidia wengi.
- **Kuwa na vipindi vya kupumzika.** Tunaweza kuchambua habari zenye kufadhaisha kwa ufanisi zaidi wakati hatujachoka.
- **Kuweka mwili katika hali nzuri.** Mazoezi, kujinyoosha, mazoezi ya kupumua, usingizi wa kutosha, lishe bora ni njia bora za kutoa kusanyiko la mafadhaiko.
- **Kuzungumza na mwenzako wa kazi, mshauri au rafiki kuhusu mambo yanayokusumbua.** Wakati

mwingine ni vigumu kufikiria vizuri bila kuongea na mtu mwingine. Ikiwa wewe ni mwenzako wa kazi anakushauri, kuwa msikilizaji mzuri badala ya kukimbilia kutatua shida hiyo kabla hawajapata nafasi ya kufanya uchunguzi. Kuandika hisia zako na uandishi wa kibinafsi pia unaweza kusaidia.

- **Kuungana na maumbile.** Watu wengi wanapata kuwa hii njia inasaidia sana.
- **Kujifunza kwa makosa yaliyotokea.** Ikiwa mambo hayaendi sawa, uwe mwenye kujifunza kutoka kwa ajali na maamuzi mabaya badala ya kuyarudia.

Mengi ya yale tumeyataja ni ya kuunda tabia za kinga na sio kuyaacha wakati mafadhaiko yanapoongezeka. Hata wakati uko uwanjani na kufanya kazi kwa masaa yasiyotabirika, kutakuwa na aina ya ratiba ambayo inaweza kutekelezeka. Utafiti unaonyesha kuwa msaada wa kijamii labda ndio sababu kubwa zaidi ya kuchangia ustahmilivu.[b] Jihadhari sana na kujitenga na aina yoyote ya dawa ya kujitibu za kupindukia, iwe kwa kupitia mihadharati au kufanya kazi kupita kiasi. **La muhimu ni kusawazisha.**

Kukubali mabadiliko

Iwe wewe ni mwanahabari wa eneo hilo au mgeni unayesafiri kwa ndege nje ya nchi nyingine, unaweza kuhisi tofauti kati ya uzuri wa maisha yako na hali ambazo wengine wanaishi jambo ambalo linafanya mabadiliko kuwa magumu sana.

Miongoni mwa wanahabari wanaofanya kazi kwenye mada hii, hisia za kukosa nguvu (kwa kutoweza kufanya zaidi kumaliza mateso) na hisia ya hatia (kwa sababu ya kurudi nyumbani) ni kawaida. Hakuna majibu rahisi kwa mitanziko aina hizi lakini wanafaidika baada ya kuzikabili. Labda unajiuliza swali hili: *“Je, kuwa mkali juu yangu kwa sababu ya mambo ambayo siwezi kudhibiti husaidia wale ninawahoji au kuunda kazi inayofaa?”* Ni vigumu kuwa na huruma kwa wengine, bila pia kuwa mwenye huruma kwako mwenyewe. Kadiri mada inakuwa ya kuhuzunisha, ni muhimu zaidi kurudi nyuma na kutafuta vitu vidogo vyema ambavyo unapata za kuridhisha. Tena, kuzungumza na watu ambao wanaelewa maswala inaweza kusaidia jambo hili.

Rasilimali za ziada: ustawi wa kibinafsi

Kituo cha Dart kina mwongozo wa kina ju ya kufanya kazi kuusu **picha za kiwewe**. Tazama pia hili habari fupi iliyoshinikizwa juu ya kufanya na **ushuhuda wa kutisha wakati wa uchunguzi wa kuzama** na **mjadala huu** juu ya utunzaji wa kibinafsi kati ya wanahabari na watengenezaji wa filamu walifanya kazi kwenye adithi za unyanyasaji wa kingono za watoto. Kama inavyo tajwa katika sehemu ya **#1**, wameneja waweza kurejelea **mwongozo huu**. Sehemu hii ya wavuti inaangalia maswala ya shirika kwa undani zaidi, pamija na jukumu la msaada wa rika.

Wacha tuzungumze: Mipaka ya kibinafsi, usalama na wanawake katika uandishiwa Habari hutoa ushauri kwa waandishi wa habari wa kike juu ya kushughulikiaunyanyasajiwa kijinsia; **karatasi hii** ya nchailiyozalishwa na kituo cha Dart Centre for RSF inatoa shauri maalum wa kujitunza kwa waandishi wa habari wanaofanya kazi katika maeneo yenye migogoro; na mwishowe hadithi za unyanyasaji wa kijinsia mara nyingi ni sumaku kwa “trolls” na watendaji wengine wabaya mkondoni – hapa kuna maoni kadhaa ya **kujilinda kwa dijiti**.

BONYEZA HAPA KUSHIRIKI SEHEMU HII:

[a] Tazama S. M. Southwick na D. S. Charney, Ustahimilivu: Sayansi ya Kusimamia Changamoto Kubwa za Maisha (Cambridge University Press, 2012) haswa sura 4, 6, na 7.

Tafadhali fikiria tu kuchapisha kurasa za nakala za greyscale

#7.

ELEZA HADITHI

KUMBUKA: UNYANYASAJI WA KIJINSIA SIO MWELEKEO PEKEE WA HADITHI KWENYE TUKIO

ELEZA HADITHI

#7. KUMBUKA: UNYANYASAJI WA KIJINSIA SIO MWELEKEO PEKEE WA HADITHI KWENYE TUKIO

Kuzingatia sana ukatili wa matukio peke yake inaweza kuleta athari mbaya kwa wale unawahoji na uandishi wa habari kwa jumla. Kuwa mwangalifu kwa muktadha kamili.

Baada ya kukabiliwa na hofu kubwa kama vile ubakaji wa watu wengi katika vita au utumikishwaji wa biashara ya ngono, mwanahabari anaweza kuhisi kama ni kawaida kuweka mwelekeo wote juu ya vurugu za kijinsia na madhara ambayo husababisha. Lakini kushindwa kuangazia muktadha mpana kunaweza kufanya ripoti yako kuwa finyo hivyo kuwapoteza watazamaji na pia kuwatenga wahasiriwa. Na kwa hivyo hakikisha kupanua ripoti yako kwa njia zifuatazo:

- **Toa maelezo kamili kuhusu maisha ya wahasiriwa. Kuwa mwangalifu usitabiri uharibifu au kudhalilisha wahasiriwa kwa mambo mabaya yaliyowapata. Jambo hili linaweza kufanya vigumu wao kupona.**
- **Fikiria kuwa kuna uhalifu mwingine zaidi ya ubakaji. Wahasiriwa wanaweza kupoteza wapendwa wao, nyumba zao, na kuhamishwa kwa nguvu. Vitu hivi ni muhimu kwa watu pia.**
- **Epuka kuzingatia kupita kiasi habari ambazo zinaweza kufanya kisa kuwa cha kingono/au cha kusisimua. Hili linaweza kupunguza huruma ya umma kwa wahasiriwa.**
- **Saidia hadhira yako kuona njia za suluhisho zinazowezekana kwa kutendae haki kwa muktadha kamili wa kisiasa na kijamii.**

Mara nyingi tunapuuza jinsi kazi yetu inaweza kusaidia wahasiriwa na hata kuwa na athari juu ya jinsi wanavyopona.

Ukatili wa kijinsia unahusishwa na viwango vya juu vya kisaikolojia na vile vile maumivu ya kimwili. Matokeo ya jeraha la kijinsia kawaida huleta hisia kali za kujitenga, ambayo watu huhisi wamejitenga na wao wenyewe – mtu aliyvokuwa kabla ya yote kutokea – na pia kujitenga na wengine. Uwezekano wa watu waliopatwa na ukatili wa kijinsia kukata uhusiano na jamii pana inaweza kuacha wahasiriwa wakiwa wametengwa na hivyo kupunguza nafasi za msaada.

Kwa upande mwingine, ili kupona inaonekana kinuyme cha hiki kinahitajika. Inatokea kupitia kuunganishwa tena, wakati watu wanaamini kuwa inawezekana tena kwa wengine kuwajali na kuwaheshimu.

Kama wanahabari, sio jukumu letu kuponya watu – na haitakuwa busara na itakuwa kama dharau kudhani kwamba kazi yetu itawasaidia wahasiriwa kwa njia ya moja kwa moja. Hata hivyo, tunapaswa kuzingatia ili tusiongeze hizo nguvu za kuvunja uhusiano bila kukusudia. Jina Moore, mwandishi wa habari wa Amerika ambaye anafanya kazi Afrika Mashariki, anaandika hivi:

> *Tunapaswa kuhakikisha kuwa hakuna chochote katika ripoti tutakayochapisha – kwa siku, miezi, na mwaka – ambayo inashangaza, inatia aibu, fedheha au inawahatarisha … Lengo la kurudia maelezo ya kisa cha cha mhasiriwa ni kuhakikisha kwamba anaelewa kile watu wengine watajua juu yake..*[a]

[a] Katika makala ya Jina Moore: **Mtego wa Ponografia**.

Ujumbe ambao tunatuma kwa hadhira iayolengwa pia ina umuhimu mkubwa. Kila mahali majadiliano kuhusu tukio la kiwewe la kijinsia yanaandamana na hadithi za uwongo, unyanyapaa na kasumba zisizo na usaidizi. Tunaweza kuziimarisha au kuonyesha ukweli kuhusu kasumba hizi- wanahabari na watengenezaji wa sinema sio watazamaji tu bila kuwa na hisia zao.

Hii ndio sababu kuwa ufahamu kamili juu ya muktadha wa kisiasa, kiuchumi, na kitamaduni wa mzozo ni muhimu.

Hatari ya kuangazia upande mmoja tu wa kisa

Tukio la ukatili wa kingono unaeza kufanyika katika aina tofauti lakini mara nyingi kitu kinachoonekana zaidi ni ukatili wake. Kama mtengenezaji wa filamu au mwanahabari, unaweza kupata hamu kali ya kusisimua hadhara inayolengwa kwa kutumia mabaya ya yale uliyosikia kwa matumaini ya kuwaamsha. Hili ni jambo linaloeleweka kabisa.

Lakini hatari iliyopo ni kwamba hii inaweza kuleta madhara. Kuzingatia sana kuhusu tukio la kutisha na undani wa ukatili wa kijinsia, kunaweza kulazimisha hadhira inayolengwa kuacha kutilia maanani na kujitenga kwa njia ambazo zinaweza hata kupunguza huruma kwa watu walioathiriwa na ukatili wa kijinsia katika migororo. Kama hakuna habari ya kutosha, hadhira inayolengwa haitaelewa hali ya uhalifu huu na ni nini kiko hatarini.

Kwa Stephanie Kariuki, ambaye alikuwa akifanya kazi na Podcast for Vice ambayo ilichunguza unyanyasaji wa kijinsia huko Misri na jukumu la serikali katika kuendelea kwake, maamuzi haya yanahitaji kusawazisha kwa uangalifu mambo haya:

> *Kulikuwa na mambo mengi kuhusu ufafanuzi wa ziada unaotakinana? Kwa nini tunatoa maelezo, na ni muhimu kweli? …. Kwa mfano, walichunguza uke wa mwanamke mara nne. Hilo ni jambo la kindani sana kutaja – na mara nne ni nambari imeambatanishwa nayo. Na sababu ya sisi kwenda kwa undani kama tunavyofanya ni kwa sababu uchunguzi huu ambao anapitia ni ishara ya kile serikali ilikuwa ikifanyia wanawake kwa miongo kadhaa.*[b]

Hakika, kuandika kwa ufanisi juu ya matukio ya kiwewe inahitaji kujua jinsi ya kusawazisha masuala tofauti ambayo yanapingana. Kwa mfano:

- **Je, ni kiasi gani mtaongea kuhusu madhara, kukosa msaada, na upotezaji wa udhibiti ambao ukatili wa kijinsia unaleta kwa maisha ya wahasiriwa? Au ni kiasi gani mtaongea kuhusu upinzani na kupona- ilihitaji nini, na inahitaji nini kuishi?**

Hata kama inaonekana mbaya, wahasiriwa wana mambo mazuri yanayoendelea katika maisha yao. Kuonyesha tu matukio ya kutisha na kutokuwa na nguvu sio jambo sahihi wala la kusaidia.

- **Je, ni kiasi gani itakuwa kuhusu matukio aliyopitia mhasiriwa na ni kiasi gani juu ya muktadha mpana – haswa hali ya kisiasa na kijamii?**

Kukosa kuzingatia kikamilifu muktadha mpana kutafanya ripoti kuwa kisa cha kuleta hisia ya kibinadamu ya aina ya kushangaza na ya kusumbua – ripoti ambayo haina lengo maalum na ambayo haiwapi hadhira inayolengwa uelewa mzuri wa kile kinachotokea na suluhisho. Ukatili wa kijinsia haufanyiki bila matukio mengine – mada kamaubakaji vitani haieleweki bila kutaja matukio yanayochochea mzozo.

Kwa upande mwingine, kutowapa watu uzingativu kamili kwa hali zao za kibinafsi pia inaweza kuonyesha kukosa heshima, kwani inaweza kutoa taswira kuwa mtu alijumuishwa tu ili kuwa kama takwimu fulani.

Kujadili mivutano inayokinzana

Kila kisa kitahitaji mizani tofauti. Kuelewa hili jambo mara nyingi ni vigumu kwa sababu ya athari ya vurugu ambayo inaweza kutupelekea kuona kila kitu hakina maana. Habari za kutisha za kiwewe huwa zinakuza fikra finyu. Ni rahisi sana kukwama kwenye maelezo au pande kidogo.

[b] Kariuki alishiriki katika utafiti wetu kuhusu suala hili.

Hapa kuna orodha fupi ya kuangalia wakati unapoandika au unahariri:

- Je, hii inaingia ndani sana katika maelezo ya picha ya kimwili au ya kibinafsi?
- Je, kuna maelezo kuhusu mwili wa mtu, muonekano, mavazi, nk, ambayo yana hatari ya kuifanya maelezo ya kingono (na hata kuidhinisha motisha ya unyanyasaji)?
- Je, kisa hiki kinaweza kutabiri uharibifu wa baadaye wa mtu au jamii? Hata kama mambo yanaonekana mabaya, sio sahihi na kuhukumu kuwa haiwezekani kupona. (Ikiwa unapata shida kuona chochote kizuri, jiulize kuna nini kizuri kwa mtu huyu zaidi ya unyanyasaji? Wanapata wapi ujasiri na msaada)?
- Kwa upande mwingine, je, ninachukua mkondo wa kinyume na kutoa matumaini ya uwongo kwa nia ya kupunguza makali ya hali mbaya? Mbali na shida iliyo wazi kuhusu usahihi, uandishi wa habari unaotilia chumvi uwezeshaji unaweza kuwatenga wale ambao hawatambui hali zao.
- Ikiwa makala yangu yanajumuisha sauti za wahusika na wahasiriwa, je, kuna chochote katika kueleza ripoti yangu ambacho kinazingatia sana kuhusu wanyanyasaji au inaongeza nguvu zao? (Kupata hili sahihi ni kazi ngumu. Kutenganisha sauti hizi kwa ripoti tofauti inaweza kuwa rahisi zaidi).
- Je, masimulizi yangu ynazingatia zaidi ubakaji na kupuuza shida zingine ambazo watu hupitia wakati wa vita na migogoro? Huenda kule wale wameona jamaa zao wakiuawa na kupoteza nyumba zao na kazi. Wanaweza kuwa ni wakimbizi wanaojitahidi kujenga maisha mapya. Vitu vyote hivi ni muhimu kwa watu, na wahasiriwa wanaweza kukosa kuelewa kwa nini mwanahabari na anachukua muelekeo wa upande mmoja.

Namna ya kueleza ripoti: maelezo kwa wahariri

Njia ambayo habari inatolewa – kichwa cha habari, maelezo mafupi ya picha, picha zinazotumiwa kutangaza filamu, muhtasari, njia inayowasilishwa kwenye mitandao ya kijamii – inaweza kuwa na athari kubwa kwa jinsi habari inapokelewa na athari yake kwa watu ambao wamehusishwa na habari hio.

Hatari moja iliyo wazi ni kuifanya ripoti ionekane kama ya ngono – kuifanya iwe ya kusisimua kwa njia ambayo inaitoa kwenye muktadha halisi. Katika ukatili wa kijinsia, ngono inaweza kutokea – lakini matukio haya sio kwa njia yoyote kama ngono ya kawaida.

Maneno kama ‘watumwa wa ngono’ ni ya kuogofya na ina hatari ya kugeuza unyanyasaji kuwa burudani. Maneno kama “bibi harusi watoto” ni vizuri ikielezewa kama “kutekwa nyara na unyanyasaji wa kijinsia wa mtoto.” Mtu ambaye amelazimishwa kufanya ukahaba sio mpenzi.

Hapa, Jineth Bedoya, ambaye ameandika sana kususu ukatili wa kijinsia huko Amerika Kusini. Anaelezea jinsi mifumo ya ukatili wa kijinsia unaofanywa na wanamgambo imefichwa nyuma ya lugha isiyofaa na ya zamani kama:

> *Tumefanya kampeni kali kwenye vyombo vya habari ili waache kutumia neno ‘uhalifu wa mapenzi’ wakati wanahabari wanataja ubakaji au mauaji ya wanawake.*
>
> *Jamii bado inatizama ubakaji kuwa unahusishwa na uchochezi wa kijinsia ambao mwanamke analenga kwa makusudi kwa mwathiriwa wake. Ndio maana kutumia neno “mapenzi.”*
>
> *Lakini kwa kweli, uchochezi hapa ni lile wazo katika aina hii ya uanahabari kwamba uhalifu kama huo unafanywa kwa jina la mapenzi.*
>
> *Katika kesi nyingi nimesikia wanaume wanaobaka wakijitetea kwa hoja hii. Wanasema kwamba “waliwanyanyasa kijinsia,” au kuwaua kwa sababu waliwapenda.*

[c] Carlos Koos (2017) Ukatili wa kijinsia katika mizozo: maendeleo ya utafiti na mapungufu iliyobaki, Ubora wa Dunia ya Tatu, yapatikana **hapa**.

Jihadhirini pia kwamba upangaji wa ubakaji kama matokeo ya kuepukiya vita ni hadithi. Mbali nakuwa uhalifu wa kivita unaostahili adhabu, utafiti unaonyesha kwamba haujaenea katika mizozo yote, hata pale wapiganaji wa kawaida.[c]

Popote unapoweza, jumuisha rasilimali za mashirika ya msaada na habari ambayo inaweza kusaidia mtu yeyote ambaye ni mhasiriwa wa ukatili wa kijinsia kusoma au kutazama kipande hicho.

Rasilimali za ziada

Katika **Mtego wa Ponografia**, Jina Moore alizungumzia changamoto za kupata lugha sawa. **Zana kutoka** kwa Kikosi cha Kazi cha Chicago juu ya Ukatili Dhidi ya Wasichana na Wanawake Vijana inajadili kuripoti kwa unyanyasaji wa kijinsia kwa jumla na ina sehemu inayoonyesha juu ya uchaguzi wa lugha.

Makala haya kutoka kwa Kituo cha Kitaifa cha Rasilimali za Ukatili wa Kijinsia na pia inashughulikia aina zote za unyanyasaji wa kijinsia huko Merikani na hainauhusiano wowote ule na Vurugu za Kijinsia zinazohusiana na migogoro, (CRSV). Lakini, inaonyesha nguvu ya kuchukua mbinu inayoongozwa na muktadha wa kitakwimu.

Kwenye wavuti ya Kituo cha Dart, **Nina Berman** aangazia umuhimu wa muktadha na juu ya kufanya upelelezi unaofaa wa kuona — haya yote yamefafanuliwa zaidi katika sehemu inayofuata.

BONYEZA HAPA KUSHIRIKI SEHEMU HII:

Tafadhali fikiria tu kuchapisha kurasa za nakala za greyscale

#8.

ELEZA HADITHI

PICHA HAZIFUTIKI: KUWA MWANGALIFU KWA PICHA UNAZOTUMIA

© Dart Centre Europe

ELEZA HADITHI

#8. PICHA HAZIFUTIKI: KUWA MWANGALIFU KWA PICHA UNAZOTUMIA

Mara tu picha zimechapishwa, haziwezi kurejeshwa tena. Ufikiaji wa wavuti kwa watu wote unaweza kuwaweka watu katika hatari za aina nyingi.

Unaporipoti kuhusu ukatili wa kijinsia katika migogoro ni muhimu kuchagua vizuri video au picha unazozitumia. Hasa sasa katika enzi ya dijitali, picha zina kaa muda mrefu kuliko visa unavyoripoti. Ni muhimu kwamba wahasiriwa waelewe kikamilifu jinsi watakavyowasilishwa kwa picha auvideo na nini matokeo yake. Unapaswa kuzingatia:

- **Je, kuna haja kubwa ya kuwatambulisha wahasiriwa au ni salama kwanza kuripoti bila wao kujulikana?**
- **Je, wametoa idhini yao halisi kupigwa picha au kuchukuliwa video? Je, wanaelewa ufikiaji wa mitandao ya kijamii ambayo inaweza kuonekana katika jamii zao?**
- **Je! Kuna kitu chochote kwenye picha ambacho kinaweza kufunua utambulisho wao bila kukusudia?**
- **Ninawezaje kuwashirikisha katika kutengeneza picha ili waridhike na nakala za mwisho?**
- **Na jambo la kimsingi la maadili: je, ningefurahi mimi au mtu wa familia yangu kupigwa picha au video hivi?**

Acha niwe wazi, picha za ubakaji katika migogoro na wahasiriwa wa ubakaji zinahitajika kusambazwa kwa wingi. La muhimu ni kupigwa kwa njia ambazo zinalinda wahasiriwa, kwamba picha zinaheshimu muktadha, picha haziendelezi kasumba potofu, na hazijawasilishwa na vyombo vya habari kama suluhisho mwafaka kwa wahasiriwa.[a]

Picha ni sehemu muhimu ya kuripoti migogoro, ikiwemo ukatili wa kijinsia katika migogoro, na inaweza kuwa njia nzuri sana ya kuleta uhusiano kwa wasomaji. Lakini pia kuna uwezekano mkubwa wa kudhuru wahasiriwa mbali na hatari ya kuwahoji.

Kuna historia ndefu ya picha za kibaguzi ambazo ni za kutoka enzi za ukoloni na utumwa na kwa hivyo kuelewa kuhusu matumizi ya picha ni muhimu.

Kwa kuongezea, Picha zinasambazwa kwa urahisi katika enzi ya dijitali, kwenye vifaa tofauti na kwenye majukwaa yote. Hii inamaanisha kwamba wahasiriwa wanaweza kusumbuliwa hata kama wanaishi vijijini na kwa miaka ijayo. Kwa mfano, katika vita vya Balkan vya miaka ya tisini, kulikuwa na visa ambavyo wanawake waliolewa bila kuwaambia waume zao kwamba walikuwa wamebakwa… Miongo kadhaa baadaye, wachache walikuwa na wazo kwamba nyenzo za kumbukumbu zinaweza bado kupatikana mtandaoni.

Enzi ya dijitali pia inatoa nafasi ya habari zinazoambatana na picha na hivyo kuleta shinikizo kwa wahariri na wapiga picha kutumia picha za kusisimua zaidi na za kuvutia. Hii inaweza kusababisha picha zinazochochea mwili wa mhasiriwa, au kuzitambulisha bila haja.

[a] Nina Berman ni mpiga picha wa maandishi ambaye ali repoti mizozo katika Boznia na Afhanistan. Yeye pia ni mhangiaji waw a utafiti wa mradi huu. Aliandika kuhusu maadili ya upigaji picha mahai za vita na za amani; na ni profesa wa uandishi wa habari katika chuo kikuu cha Coumbia. Kwa zaidi angalia: **https://dartcenter.org/resources/visual-choices-covering-sexual-violence-conflict-zones**

Linapokuja suala la wahasiriwa wa ukatili wa kijinsia katika migogoro, vielelezo vya picha ni kawaida – kuonyesha mhasiriwa akiwa ametengwa na kufanyiwa ukatili, ametolewa kutoka kwa mazingira yao, au kuzingatia sana mwili wake.

Kama ilivyojadiliwa hapo awali katika kifungu cha **#3** kuhusu idhini, kuwashirikisha waliohojiwa katika maamuzi kuusu jinsi wataonyeshwa,h ni mazoezi mazuri. Wanahabari wakiripoti kuhusu ubakaji wa wanawake wa Yazidi na ISIS waldhani walihakikisha kutojulikana kwa wanawake hao kwa kuwapiga picha wakiwa wamefunikwa nyuso, lakini kwa kweli, walikuwa wakitambulika kwa urahisi ndani ya jamii zao kwa macho yao na mitandio tofauti.

Kufanya uchaguzi mzuri zaidi na maadi ya kuona

Ingawa wapiga picha wa vyombo vya habari mara nyingi wanafanya kazi na shinikizo kutoka kwa ofisini ili kupata picha yenye athari zaidi, inawezekana kuchukua picha za wahasiriwa wa ukatili wa kijinsia ambazo zinaweza kuepusha madhara kwa mhojiwa hata kama wakati ni mchache. Hapa kuna maswali ya kujiuliza juu ya picha unazochukua:

- Je, unaweza kuanza na dhana kwamba picha zozote za wahasiriwa hazitajulikana, na kwamba watatambuliwa tu ikiwa kuna sababu kubwa ya kufanya hivyo? Jadili jambo hili kwa undani na mhariri wako kabla ya kufika unakoenda.
- Kuna njia nyingi imara na za ubunifu za kuchukua picha ambazo haziwatambulishi wahasiriwa. Ni bora kufikiria haya mapema kabla ya wakati. Labda uanaweza kuweka albamu ya dijitali kama wengine wanavyofanya.
- Kwa kuwa ripoti hiyo inahusu ubakaji, unapaswa kufahamu jinsi unavyoonyesha mwili wa mhasiriwa. Je, ni sehemu gani ya mwili unayotaka ionekane na ni jinsi gani unaweza kuzuia kuonekana kwa mhasiriwa kama kitu cha ngono?
- Jaribu kutafuta njia inayoepuka picha ambazo zinazoonyesha kuwa mhasiriwa ni mpweke au ameangamizwa. Wakati mwingine fikra ya kutengwa sana inaweza kuwa ndio ukweli wa mambo, lakini kawaida watu huwa na muktadha mpana wa msaada – na ni vizuri zaidi kuonyesha hilo.

Ikiwa unatumia mbinu za dijiti kuficha utambulisho, saizi asili zinahitaji kuondolewa kutoka kwenye picha, sio tu kuwa ukungu; na kwa kweli, hakikisha kuwa hakuna data meta katika faili ambayo inabainisha eneo. Ni muhimu pia kufikiria ni nani anaweza kuwa karibu wakati picha zinachukuliwa na kwanini? Hapa kuna vidokezo vya kuzingatia:

- Je, anayehojiwa angependa kuwa na mtu pamoja naye au kuna watu ambao hawapaswi kutazama? Kwa watengenezaji wa filamu, jaribu kupunguza wasaidizi wa kazi.
- Baada ya picha hizo kuchukuliwa, ni vizuri kuwaonyesha wahasiriwa ili kuwaruhusu waeleze ikiwa wanaridhia na vile picha zimepigwa.
- Hakikisha wahasiriwa wanaelewa kuwa picha zao zinaweza kudumu kwa muda mrefu sana na kwamba zinaweza kusambazwa kwenye majukwaa mengi yakiwemo katika jamii yao.

Je, kuna njia za kutokuharakisha kazi hio? Je, unaweza kujadili jinsi upigaji picha utafanya kazina kuelezea itachukua muda gani? Kumbuka kwamba watoto hawawezi kamwe kutoa idhini ya kuonyesha utambulishi wao hata kama mtu mzima ametoa idhini.

Uanahabari wa picha na Wahariri

> ***Ninaweza kuelewa jinsi mpiga picha anavyoweza kukosa kufahamu haya, lakini sitarajii hilo kutoka kwa mhariri. Ninahisi kuwa kwa wahariri wana uwajibikaji zaidi wa kuelewa kuhusu picha kulingana na muktadha wa kihistoria.***
> *Nina Berman.*[a]

Wapiga picha huwa na uhusiano na wahasiriwa na hufanya maamuzi kuhusu matumizi ya picha. Lakini wahariri hubeba jukumu la mwisho kwa picha ambazo zimeagizwa na kuchaguliwa kutoka kwa picha nyingi kabla ya kufikia umma. Kinachoweza kufaa kwa ukarasa wa ndani – ambapo ina maana na muktadha – inaweza kuwa na athari tofauti kabisa ikiwa inasimama peke yake kwenye kifuniko au chapisho la Instagram.

Kwa kutumia utaalam na wakati wa kufikiria kimkakati mbali na shinikizo za uwanjami, wahariri wanapaswa kuzingatia namna ya picha itaonyeshwa kwa makusudi au bila kukusudia. Kwa mfano, kuna historia ndefu ya picha za watumwa ambazo waandishi wa habari wanaofanya kazi katika nchi zinazoendelea wanapaswa kuziepuka.

Wahariri wa picha wanaweza pia kuwa na nguvu ya kufanya maamuzi juu ya nini kittendeka baadaye kwa picha – leseni yake na upatikanaji – na pia njia ambayo inatumika kwenye mitandao ya kijamii.

Wahariri, Wanaweza kuwa wamefanya kazi na wafanyikazi wenzao wa muda mrefu, au kuwaagiza wapiga picha huria ambao hawajawahi kukutana nao. Kupata wakati wa mazungumzo mafupi ya dakika 10 juu ya mipaka, idhini halisi, na kutokujulikana kunaweza kuleta mabadiliko makubwa.

Hapa kuna mambo ya kuzingatia:

- Je! umekuwa na mazungumzo yakutosha na wapiga picha kuhusu idhini?
- Je! kuna haja ya wahasiriwa kutambuliwa? Je, aina gani ya picha utatumia wakati wa kuhifadhi kutokujulikana?
- Maelezo mafupi ya picha ni sehemu ya ripoti na kama picha, hayapaswi kumdunisha au kumnyanyapaa mtu huyo.
- Je! unaweza kutoa muda wa picha za wahasiriwa wa ukatili wa kijinsia katika migogoro? Je, unaweza kuzifanya zitumike mara moja tubila kuuzwa kwa wakala?
- Je, picha hizo zitatumiwaje kwenye mitandao ya kijamii? Je, unahitaji kuonyesha uso au mwili wa mhasiriwa kwenye Instagram, kwa mfano, au kuna njia nyingine ya kuhamasisha kisa, yenye haimwachi mtu aliye hasiriwa kubeba uzito wake wote?

BONYEZA HAPA KUSHIRIKI SEHEMU HII:

[a] Nina Berman ni mpiga picha wa maandishi ambaye ali repoti mizozo katika Boznia na Afhanistan. Yeye pia ni mhangiaji waw a utafiti wa mradi huu. Aliandika kuhusu maadili ya upigaji picha mahai za vita na za amani; na ni profesa wa uandishi wa habari katika chuo kikuu cha Coumbia. Kwa zaidi angalia: **https://dartcenter.org/resources/visual-choices-covering-sexual-violence-conflict-zones**